# NURU
# YA
# KURANI

## Toleo la Kwanza


Na

Hadhrat Mirza Ghulam Ahmad[as] wa Qadian
Masihi Mau'udi na Imam Mahdi

ISLAM INTERNATIONAL PUBLICATIONS LTD

**Nuru ya Kurani Toleo la Kwanza**

Tafsiri ya Kiswahili ya: Noorul-Qur'an No. 1 (Kiurdu)
Noorul-Qur'an No. 1 (Swahili Translation)

**Mwandishi:**
Hadhrat Mirza Ghulam Ahmad[as] wa Qadian

**Mfasiri:**
Sheikh Abid Mahmud Bhati

Chapa ya Kwanza (Kiurdu): 1895
Chapa ya Kwanza (Kiswahili): 2021

© Islam International Publications Ltd.

**Kwa Maelezo Zaidi:**

**Tanzania:**
Jumuiya ya Waislamu Waahmadiyya, Tanzania
Mtaa wa Bibi Titi Mohamed S.L.P. 376, Dar es Salaam.
Simu: +255222110473 Fax: +255222121744

**Kenya:**
E.A. Ahmadiyya Muslim Mission
P.O. Box 40554 Nairobi Kenya Simu: +254222111031
Kimechapwa na Ahmadiyya Printing Press
Dar es Salaam, Tanzania / Nairobi, Kenya

**ISBN:** 978-1-84880-220-9
10 9 8 7 6 5 4 3 2 1

## Neno la Mbele

Mnamo mwaka 1958, Mwanzilishi wa Jumuiya ya Waislamu Waahmadiyya, Hadhrat Masihi Mau'udi[as], alinuia kutoa jarida moja, 'Nurul Kuran', litakalochapishwa baada ya kila miezi mitatu ili kuvavagilisha sifa kamilifu za ruhania ya Kurani Tukufu na mambo yaelezayo falsafa ya kweli ya kuzituliza nyoyo.

Lakini kazi nyingine nyingi za dini zilimshughulisha sana na akaweza kutoa matoleo mawili tu ya jarida hili. Toleo la kwanza lilikuwa kwa miezi mitatu, Juni, Julai na Agosti 1895, na toleo la pili kwa miezi minane, yaani Septemba 1895 hadi Aprili 1896.

Mbele yenu wakati huu ndio toleo la kwanza la Nurul Kuran alilofasiri kwa Kiswahili Sheikh Abid Mahmud Bhatti; kisha Sheikh Muzaffar Ahmad Durrani akaidurusu. Kabla haijapelekwa mtamboni kuchapishwa nikaisoma kwa makini na kujaribu nilivyoweza kuisogeza karibu zaidi na lugha chanzi.

Sheikh Ansar Hussain akazipanga herufi zake kwa kompyuta na kutayarisha fometi. Wahusika wote wanastahili kuombewa kuwa Mwenyezi Mungu Awape malipo bora. Mola wangu Awanufaishe wasomaji wote kiroho na kielimu. Amin.

Jamil R. Rafiq
Wakilut-Tasnif
Tahrike Jadid
Rabwah, Pakistan

20 Julai 2020

ٹائیٹل بار اوّل

اِنَّ الدِّیْنَ عِنْدَ اللّٰہِ الْاِسْلَام

# نور القرآن

## اطلاع

یہ رسالہ نور القرآن بالفعل تین ماہ کے بعد یعنی چوتھے مہینے شایع ہوا کریگا

اور یہ نمبر تین ماہ یعنی **جون۔ جولای۔ اگست** ۱۸۹۵ء کے بابت ہے

قیمت بالفعل وہی **ایک** روپیہ سالانہ ہے

راقم خاکسار سراج الحق جمالی نعمانی

در مطبع ضیاء الاسلام قادیان حکیم فضل دین صاحب بھیروی کی اہتمام سے چھپا

Jalada la chapa ya kwanza

Bila shaka dini hasa
mbele ya Allah ni Islam

# Nuru ya Kurani

## Tangazo

Jarida hili litakuwa linachapishwa kila baada ya miezi mitatu katika mwezi wa nne. Na toleo hili ni kwa miezi mitatu hii, yaani Juni, Julai na Agosti 1895. Na bei yake ni Rupia moja kwa mwaka.

Mtangazaji Mnyenyekevu: Siraj-ul-Haq Jamali Nu‘mani.

Limechapishwa katika
Matbaa Dhiya’ul Islam Qadian,
chini ya usimamizi wa
Hakim Fadhl Din Bherawii.

بِسْمِ اللّٰهِ الرَّحْمٰنِ الرَّحِيْمِ[1]
نَحْمَدُهٗ وَنُصَلِّيْ[2]

# TANGAZO

## Kuhusu kitabu cha "Minanur Rahman"

Hiki ni kitabu cha ajabu sana ambacho baadhi ya aya za Kurani Tukufu zilizojaa hekima, zimetuelekeza kukiandika. Hivyo, hii pia ni ihsani kubwa ya Kurani Tukufu kwa dunia ya kwamba imeeleza mzizi wa tofauti za lugha mbalimbali, na imetufahamisha jambo hili nyeti kuwa lugha zote za wanadamu zimetokana na chanzo na chimbuko gani, na kwa jinsi gani walikuwa wamedanganyika wale watu wasiokubali kuwa asili ya lugha ya wanadamu ni hii kwamba imefundishwa na Mwenyezi Mungu. Na ibainike kuwa imethibitishwa ndani ya kitabu hiki sawa na utafiti wa lugha kwamba katika dunia Kurani Tukufu ndio kitabu cha pekee kilichoteremshwa katika lugha iliyo mama wa lugha zote na ni lugha ya ufunuo, na chanzo na chemchemi ya lugha zote. Jambo hili liko wazi kwamba uzuri na ubora wa kitabu cha Mwenyezi Mungu umo katika jambo hili ya kuwa kiwe katika lugha itokayo kinywani mwa Mwenyezi Mungu na katika sifa zake izishinde lugha zingine zote na iwe kamili katika mpangilio wake. Na tukikuta ukamilifu huo katika lugha fulani, ambao

---

[1] Kwa jina la Allah, Mwingi wa Rehema, Mwingi wa Ukarimu.

[2] Tunamsifu Yeye (Allah) na tunamsalia (Mtume[saw]).

nguvu za binadamu na ubainifu wa mtu unashindwa kuutia ukamilifu huo ndani ya lugha hiyo, na tushuhudiapo sifa njema ambazo zinakosekana katika lugha zingine, na kuziangalia sifa maalumu ambazo minghairi ya elimu ya tangu azali na sahihi ya Mwenyezi Mungu, hakuna akili ya mahuluku yeyote awezaye kuzibuni, hapo tunalazimika kuamini ya kwamba lugha hiyo inatokana na Mwenyezi Mungu. Hivyo, kutokana na utafiti kamilifu wa kina imefahamika kuwa lugha hiyo ni Kiarabu. Ingawa watu wengi wamefanya utafiti huu maisha mazima kufanya juhudi sana kwa kugundua kuwa mama wa lugha zote ni ipi. Kwa kuwa juhudi zao hazikuwa kwenye mstari ulionyooka, na pia hawakusaidiwa na Mwenyezi Mungu, kwa hiyo hawakufanikiwa. Na hii pia ilikuwa sababu kwamba hawakushughulikia barabara lugha ya Kiarabu bali kulikuwa na ubahili wa aina fulani, hivyo hawakuweza kutambua uhakika ulivyo. Sasa kwa kupitia Neno Takatifu la Mwenyezi Mungu, Kurani Tukufu, tumeongozwa kwenye jambo hili kuwa ile lugha iliyofunuliwa na iliyo mama wa lugha zote ni lugha ya Kiarabu — ambapo Wazorosta kwa upande wao, Waebrania kwa upande wao na Waaria kwa upande wao wamedai kuwa lugha yao ndiyo mama wa lugha zote, ilhali wote waliotoa madai hayo wamekosea. Ingawa sisi hatujadhihirisha hii rai ya juu juu tu, bali kwa upande wetu tumefanya utafiti wa kina na kwa kulinganisha nayo maelfu ya maneno ya Kisanskriti na

kusikiliza toka kwa mabingwa wa lugha mbalimbali na baada ya kulizamia jambo hili tumefikia uamuzi huu kuwa mbele ya lugha ya Kiarabu, lugha zingine kama vile Kisanskriti n.k. hazina sifa yoyote ya ubora, bali kulinganishwa na maneno ya lugha ya Kiarabu maneno ya lugha hizo ni kama vilema viwete, vipofu, viziwi, yenye jedhamu na ukoma, ambayo yamepoteza mpangilio wa asili na pia hayana hazina ya kutosha ya maneno ambayo ni sharti ya lazima kwa lugha iliyokamilika, lakini kama sawa na maoni ya Mwaria au padre fulani sisi tuna makosa na utafiti wetu huu sio sahihi kwa sababu hutuzijui lugha hizo, basi kwanza jawabu letu ni kwamba kwa njia tuliyoamua jambo hili haikuwa lazima kwetu kujua vizuri maandiko ya Kisanskriti na lugha nyinginezo. Tulihitaji tu maneno matupu — siyo maneno ambatani — ya lugha ya Kisanskriti na lugha nyinginezo. Nasi tumeishakusanya hazina kubwa ya maneno haya na tumefanya utafiti wa maana zao, kadiri tulivyoweza, kutoka kwa wataalamu wa Mabaniani na kundi kubwa la mabingwa wa Ulaya wa lugha mbalimbali na tumesikiliza kwa umakini vitabu vya wahakiki Waingereza na tumeyachambua ndani ya majadiliano, kisha tumepata uthibitisho kutoka kwa wasomi wa Kisanskriti cha Maveda na lugha mbalimbali mpaka tukawa na yakini kwa njia hizo kwamba kwa hakika Kisanskriti na lugha zingine hazina zile sifa za ubora zilizothibitika katika lugha ya Kiarabu.

Jawabu la pili ni hili kwamba kama kuna Mwaria au mpinzani mwingine yeyote asiyekubaliana na utafiti wetu huu, basi tunawaarifu kwa njia ya tangazo hili kwamba katika kitabu chetu hiki tumeandika kwa marefu na mapana dalili za fadhila ya Kiarabu na ukamilifu wake na ubora wake kuliko lugha zote, ambao maelezo yake ni kama ifuatavyo.

1. Mpangilio wa maneno ya Kiarabu ni kamili.
2. Kiarabu kina sababu za kielimu za hali ya juu za nomino, jambo ambalo si la kawaida.
3. Silsila ya mfuatano wa herufi za asili za Kiarabu ni timilifu, kamilifu.
4. Katika miundo ya sentensi za lugha ya Kiarabu kuna maneno machache lakini maana nyingi.
5. Lugha ya Kiarabu ina uwezo wote wa kutoa taswira kamili ya dhamira za mwanadamu.

Sasa baada ya kuchapishwa kwa kitabu chetu hiki, kila mmoja anayo hiari kwamba kama ikiwezekana athibitishe sifa hizi za ubora katika Kisanskriti au katika lugha nyingine. Au baada ya kumfikia tangazo hili atujulishe kuhusa dhamira yake kwamba jinsi gani anataka kujiridhisha kuhusu jambo hili. Au kama anacho kipingamizi chochote kuhusu fadhila hizi au kama anakusudia kueleza baadhi ya sifa za kipekee, za Kisansikriti basi anaweza kueleza nasi tutamsikiliza kwa makini. Lakini kwa kuwa mara nyingi wanakuwepo watu

wenye wasiwasi katika kila jamii ambao hufikiria kwamba huenda katika Kisanskriti na lugha nyinginezo kuna sifa fulani za ubora zilizofichika wanazozijua wale tu wasomao vitabu vya lugha hizo na kuvifundisha, kwa hiyo katika kitabu hiki tumechapisha tangazo la zawadi ya Rupia 5000, na Rupia hizi elfu tano si maneno tu matupu, bali baada ya kupokea maombi ya Mwaria yeyote au mtu mwingine, fedha hizi zitawekwa mahala fulani anaporidhia yule Mwaria au mtu mwingine ambapo atapokea bila ya upingamizi katika hali ya kupata ushindi. Lakini ikumbukwe ya kwamba barua ya maombi ya kuweka pesa hizo yaletwe pindi kitabu cha utafiti wa lugha kitakapokuwa kimeishaenezwa baada ya kuchapwa. Na mtu huyo atakayeomba kuweka fedha atalazimika kutoa ikirari kwa maandishi kuwa baada ya kuwekewa Rupia elfu tano, kama atakwepa kushindana au hataweza kufikisha upuuzi wake hadi mwisho basi atalipa hasara yote ambayo hulipwa katika hali ya fedha za kibiashara kuwekwa bure kwa kipindi fulani.

Amani iwe kwa yule afuataye mwongozo.

Mtangazaji:

Ghulam Ahmad Qadiani.

15 Juni 1895

بِسْمِ اللهِ الرَّحْمٰنِ الرَّحِيْمِ[3]
نَحْمَدُهُ وَنُصَلِّي[4]

# MWONGOZO

Kwa sababu katika zama hizi fikra potofu za aina mbalimbali zimezagaa katika kila jamii kwa njia ambayo matokeo yake mabaya yanawafikisha hadi mauti watu wale wa kawaida wasio na taswira ya falsafa ya dini kikamilifu au taswira hiyo ni ya kubabaisha ambayo wasiwasi wa hoja potofu waweza kuifuta haraka, kwa hiyo kuihurumia hali ya zama hizi nimependelea kuandika katika jarida hili la kila mwezi yale mambo ambamo yawe tiba ya kutosha kwa maafa haya na kuwa sababu ya kuijua, kuifahamu na kuitambua njia ya kweli na, kupitia kwake ijulikane falsafa ya kweli inayotuliza mioyo na kuiletea roho utulivu na raha na kuileta imani kwenye hali ya utambuzi wa kweli. Na kwa kuwa dhamira ya utungo huu ni hii hii kwamba watu wapate maarifa na hekima za ndani za Neno la Mungu, ndio maana katika jarida hili imedumishwa kwamba pasiwepo na madai na hoja yoyote toka kwangu bali haya yote yatokane na Kurani Tukufu ambayo ni Neno la Mwenyezi Mungu na imekuja kuondoa kiza cha dunia hii, ili watu waelewe kuwa hii sifa mahususi ya kimuujiza imo ndani ya Kurani Tukufu pekee kwamba hueleza

---

[3] Kwa jina la Allah, Mwingi wa Rehema, Mwingi wa Ukarimu.

[4] Tunamsifu Yeye (Allah) na tunamsalia (Mtume)

yenyewe madai yake na hoja yake. Na hii ndio alama ya kwanza kabisa ya kutoka kwake kwa Mwenyezi Mungu kwamba huleta yenyewe ithibati yake kwa kila upande; yenyewe hutoa madai halafu yenyewe huleta hoja zake. Nasi tumependa kuchapisha sifa hii teule ya kimuujiza ya Kurani Tukufu katika jarida hili ili kwa kupitia njia hii zichunguzwe dini zile zote ambazo wafuasi wao wanavisifu Vitabu vyao visivyokuwa na nguvu hii ya kuweza kuthibitisha vyenyewe madai yao kwa kuleta hoja. Ni dhahiri ya kwamba alama ya kwanza ya Kitabu cha Mwenyezi Mungu ni nguvu yake ya kielimu. Na jambo hili haliwezekani katu ya kuwa kitabu fulani kiwe kimefunuliwa kisha kishindwe kueleza ukweli wowote ambao ni katika mahitaji ya itikadi za dini, au kwa kulinganishwa na utungo wa binadamu kiwe kimeanguka katika shimo la kiza na dosari. Bali alama ya kwanza ya Kitabu cha Mungu ni hii hii ya kuwa kiwe kinauthibitisha kimantiki pia ule msingi wa unabii na itikadi kilichouweka. Kwani, kama hakithibitishi madai yake, bali chambumbuaza binadamu, basi kukiaminisha kitabu cha namna hii itakuwa ni jambo la karaha na kulazimisha. Na jambo hili ni dhahiri na lafahamika haraka kwamba kitabu kilicho cha Mungu kwa kweli, hakitilii uzito tabia za binadamu wala hakielezi mambo yaliyo kinyume na akili, ambayo kuyakubali ndiyo karaha na kulazimishwa, kwa sababu akili timamu haiwezi kukubali kwamba karaha na kulazimishia ni halali katika dini. Nido maana, Mwenyezi Mungu

Mtukufu Amesema katika Kurani Tukufu لَآ اِكْرَاهَ فِى الدِّيْنِ[5] . Tunapotafakari kwa uadilifu kuwa Kitabu cha Mungu kinatakiwa kiweje, nuru ya moyo wetu inashuhudia kwa nguvu sana kwamba wasifu hasa wa Kitabu cha Mwenyezi Mungu ni huu kwamba kiwe kinaongoza chenyewe kielimu na kimatendo kwa nuru yake kwenye njia ya haki yenye yakini na kiimarishe mfano wa maisha ya peponi katika dunia hii hii kwa kujaalia busara kamilifu. Kwani, muujiza ulio hai wa Kitabu cha Mungu ni huu huu tu kwamba kiwe kinafundisha elimu, hekima na falsafa ya kweli, na ziwepo ndani mwake kweli zote za ruhania ambazo mwenye kutafakari anaweza kuzigundua. Tena kisiwe kinatoa madai tu, bali kithibitishe kila dai lake kwa namna inavyotuliza kabisa, na kikiangaliwa kwa mtazamo wa kina na kuzingatia barabara, ionekane wazi kuwa kwa hakika ndani mwake mna muujiza wa aina hii hii kwamba kukuza busara za mtu katika mambo ya dini kinatoa msaada wa hali ya juu na chenyewe ni wakili wa mambo yake.

Mwishowe ninamtanabahisha waziwazi kila mpinzani wangu kwa kumwambia kuwa ikiwa wao wanaviamini vitabu vyao vimetoka kwa Mungu na wanayakini vimetoka kwake Yule Aliyekamilika Ambaye Hapendi Kitabu chake Kitakatifu kipate fedheha na aibu ya kuonekana kuwa ni mkusanyiko wa madai matupu ya

[5] Hakuna karaha katika dini. Al-Baqara, 2:257

kipuuzi yasiyo na dalili yoyote, basi wao nao pia walete dalili zao kuzikabili dalili zetu. Kwani, mambo yanapokabiliana ukweli unaeleweka haraka. Na kwa malinganisho ya vitabu vyote viwili, tofauti inadhihirika baina ya kilicho dhaifu na kilicho madhubuti, na chenye kasoro na kilichokamilika. Lakini kumbukeni msiwe mawakili ninyi wenyewe, bali leteni madai na dalili zake kutoka katika kitabu chenu kama tufanavyo sisi. Na kwa kuhifadhi taratibu za majadiliano mjilazimishe kuonyesha kutoka katika Kitabu chenu kwa kuandika ndani ya jarida lenu dalili ile tunayoanza sasa. Kwa neno zima, kila baada ya kutoka toleo letu, leteni dalili ya aina ile ile iliyomo katika toleo letu, kwa kutetea Kitabu chenu. Kwa utaratibu huu, uamuzi utapatikana haraka kwamba kati ya vitabu hivi, ni kipi kinachothibitisha chenyewe ukweli wake na kinajumuisha ndani mwake bahari isiyo na kikomo ya maarifa. Sasa kwa kuwezeshwa na Mwenyezi Mungu twaanza toleo la kwanza, na twamwomba Mwenyezi Mung, "Ewe Mola Wetu, Uushindishe ukweli na udhihirishe kudhalilika na kushindwa kwa uongo.

وَلَا حَوْلَ وَلَا قُوَّةَ إِلَّا بِاللّٰهِ الْعَلِيِّ الْعَظِيْمِ ـ اٰمِيْن[6]

[6] Hakuna nguvu yoyote wala uwezo isipokuwa kwa Allah Aliye Juu, Mkuu. Amin

## UTHIBITISHO WA KWANZA

## Dalili Juu ya Kurani Tukufu na Unabii wa Mtume[saw]

Kurani Tukufu imedai kwa nguvu zote kuwa ni Neno la Mungu, na Hadhrat Seyidna na Maulana Muhammad[saw] ni Mtume na Nabii Wake wa kweli ambaye ameteremkiwa Neno lile Takatifu. Dai hili limeelezwa waziwazi sana katika aya zifuatazo:

الٓمّٓ اللّٰهُ لَآ اِلٰهَ اِلَّا هُوَ الْحَیُّ الْقَیُّوْمُ نَزَّلَ عَلَیْكَ الْكِتٰبَ بِالْحَقِّ[7] Yaani, Yeye ndiye Allah, hakuna aliye sawa naye. Uhai wa kila mmoja na uwepo wake unatokana Naye. Yeye Amekuteremshia Kitabu kwa haki na sawa na haja ya kweli. Kisha Akanena يٰٓاَیُّهَا النَّاسُ قَدْ جَآءَكُمُ الرَّسُوْلُ بِالْحَقِّ[8] (Juzu ya 5, Sura An-Nisaa). Yaani, Enyi watu! Amewafikieni Nabii huyu kwa haki na sawa na haja ya kweli. Akasema tena وَ بِالْحَقِّ اَنْزَلْنٰهُ وَ بِالْحَقِّ نَزَلَ[9] (Juzu ya 15). Yaani, Tumeliteremsha Neno Hili kwa mahitaji ya haki na limeteremka kwa mahitaji ya haki. Na vile vile Akasema, یٰٓاَیُّهَا النَّاسُ قَدْ جَآءَكُمْ بُرْهَانٌ مِّنْ رَّبِّكُمْ وَ اَنْزَلْنَآ اِلَیْكُمْ نُوْرًا مُّبِیْنًا[10] (Juzu ya 6, Sura An-Nisaa). Enyi watu, imewafikieni ithibati hii ya yakini nasi Tumewateremshieni nuru dhahiri. Na Akasema tena قُلْ یٰٓاَیُّهَا النَّاسُ اِنِّیْ رَسُوْلُ اللّٰهِ اِلَیْكُمْ جَمِیْعًا[11] (Juzu ya 9). Yaani, uwatangazie watu, mimi nimewajieni nikiwa

---

[7] Aali 'Imraan, 3:2-4
[8] An-Nisaa, 4:171
[9] Banii Israaiil, 17:106
[10] An-Nisaa, 4:175
[11] Al-Aa'raaf, 7:159

Mtume kwenu wote. Kisha Akanena وَ الَّذِيْنَ اٰمَنُوْا وَ عَمِلُوا الصّٰلِحٰتِ وَ اٰمَنُوْا بِمَا نُزِّلَ عَلٰى مُحَمَّدٍ وَّ هُوَ الْحَقُّ مِنْ رَّبِّهِمْ ۙ كَفَّرَ عَنْهُمْ سَيِّاٰتِهِمْ وَ اَصْلَحَ بَالَهُمْ [12] (Juzu ya 26). Yaani, wale watu walioamini na kufanya vitendo vizuri na wakaamini Kitabu kilichoteremka juu ya Muhammad[saw] nayo ndiyo haki, Mwenyezi Mungu atawaondolea dhambi zao na Atastawisha hali yao.

Kadhalika zipo mamia ya aya zingine ambamo imedaiwa kwa uwazi sana kwamba Kurani Tukufu ni Neno la Mungu, na Hadhrat Muhammad[saw] Mteule ni Nabii wake wa kweli, lakini twaona yafaa na yatosha kuandika kiasi hiki. Lakini papo hapo tunawakumbusha wapinzani wetu kwamba kadri yalivyotolewa madai hayo kwa nguvu sana katika Kurani Tukufu katu hayamo katika kitabu kingine kiwacho chochote. Tunayo shauku kubwa kwamba Waaria wathibitishe kutoka katika Maveda yao kwa akali kwamba Maveda yao yote manne yamedai kuwa ni Neno la Mungu, na kueleza bayana kuwa yamewateremkia watu fulani katika zama fulani. Jambo la kwanza linalolazimika kuthibitisha kuwa hiki ni Kitabu Cha Mungu ndio kwamba kitabu hicho chenyewe kidai kwamba kimetoka kwa Mungu. Kwani, kitabu kisichoashiria chenyewe kuwa kimetoka kwa Mungu, kukihusisha na Mwenyezi Mungu Mtukufu ni kiingilia kati pasipo sababu.

[12] Muhammad, 47:3

Sasa, jambo la pili lifaalo kutajwa ni kwamba Kurani Tukufu haikudai tu kutoka kwake kwa Mwenyezi Mungu na kuhusu Utume wa Muhammad[saw], bali vilevile imethibitisha madai hayo kwa dalili madhubuti na zenye nguvu. Nasi, Mungu Akipenda, tutaziandika mfululizo dalili hizi zote. Na dalili ya kwanza miongoni mwa hizo tunaiandika katika makala hii ili watafutao haki walinganishe Kurani Tukufu na Vitabu vingine kwanza katika dalili hii hii. Aidha tunamkaribisha kila mpinzani kwamba ikiwa njia hii ya uthibitisho ambayo kupatikana kwake katika Kitabu chochote ni dalili ya wazi ya ukweli wake, pia inapatikana kuhusu Vitabu vyao na manabii wao, basi wao hawana budi kuleta kupitia magezeti na majarida yao, waila watalazimika kukiri kwamba Vitabu vyao vinakosa uthibitisho wa kiwango cha juu. Nasi tunasema kwa yakini na uthabiti kwamba njia hii ya uthibitisho haipatikani katu katika dini yao. Ikiwa sisi tumekosea basi wathibitishe kosa letu. Na hoja ile ya kwanza ambayo Kurani imeileta kuhusu kutoka kwake kwa Mwenyezi Mungu, maelezo yake ni haya kwamba kwa kuamini Kitabu cha kweli na Mtume wa kweli atokaye kwa Mwenyezi Mungu, akili timamu inaipa umuhimu mkubwa hoja hii kwamba kudhihiri kwao kutokee katika zama za kiza, na watu wawe wameshika ushirikina badala ya Tauhid, ufasiki badala ya utakaso, dhulma badala ya uadilifu na ujahili badala ya elimu. Na isikike haja kali ya msuluhishi mmoja. Kisha Mtume huyu aondoke duniani ambapo

ameishafanya kazi yake ya usuluhishi kwa ufanisi mkubwa; na pia awe amelindwa na maadui zake, mpaka amalizapo kazi yake ya marekibisho; na awe amekuja kama watumishi kwa amri na kurudi kwa amri. Almuradi, adhihirike katika wakati ambapo hali ya wakati huo ipaze sauti kwamba hakuna budi kuja kwa Msuluhishi na Kitabu kutoka mbinguni. Kisha aitwe kurudi sawa na bishara ya kiufunuo ambapo awe ameishaustawisha mmea wa usuluhishi, mapinduzi makubwa yawe yamekwishadhihiri. Sasa, kwa fahari kubwa tunaeleza kwamba jinsi ilivyodhihirika hoja hii kwa sura ing'aayo kuhusiana na Kurani Tukufu na Mtume wetu Mtukufu[saw] haikuwahi kudhihiri vile kwa ajili ya Nabii yeyote mwingine wala Kitabu. Mtume[saw] alidai kwamba mimi nimekuja kwa ajili ya mataifa yote, kwa hiyo Kurani Tukufu imeyalaumu mataifa yote ya kwamba yametumbukia katika ushirikina, ufasiki na maovu ya aina aina, kama isemavyo ظَهَرَ الْفَسَادُ فِي الْبَرِّ وَ الْبَحْرِ[13], Yaani zimechafuka bara na bahari. Kisha inasema لِيَكُوْنَ لِلْعٰلَمِيْنَ نَذِيْرًا[14], yaani, sisi tumekutuma ili uyaonye mataifa yote, yaani uwatanabahishe kuwa wao wamekuwa wenye dhambi mbele ya Mwenyezi Mungu, kutokana na maasi yao na itikadi zao.

Ikumbukwe ya kuwa neno "*Nadhiir*" lililotumika katika aya hii kuhusu madhehebu yote ya dunia, ambalo

[13] Al-Ruum, 30:42
[14] Al-Furqaan, 25:2

lamanisha kuwaonya wenye dhambi na waovu, yafahamika kwalo kwa yakini kwamba Kurani ilidai kuwa dunia nzima imeharibika, na kila mmoja ameacha njia ya ukweli na wema, kwa sababu onyo ni kwa ajili ya mafuska, washirikina na waovu tu. Na kutahadharisha na kuonya huwa kwa ajili ya kuwatanabahisha wakosefu, si kwa ajili ya watu wema. Kila mmoja anatambua kwamba daima waasi na wasio waaminifu huwa wanaonywa. Na suna ya Mungu ndiyo hii kwamba Manabii huwa watoaji wa habari njema kwa watu wema, na waonyaji kwa wakosefu. Basi, kama Nabii mmoja anapokuwa mwonyaji kwa dunia nzima, hapo inalazimika kukubali kuwa Wahyi wa Nabii huyo ameilaumu dunia nzima kutumbukia katika maovu. Na haya ni madai yasiyofanywa na Torati kumhusu Musa, wala na Injili kuhusu zama za Isa[as], bali Kurani Tukufu pekee ndiyo iliyodai haya. Kisha ikasema وَ كُنْتُمْ عَلٰى شَفَا حُفْرَةٍ مِّنَ النَّارِ[15] . Yaani kabla ya ujaji wa Nabii huyu, nyinyi mlikuwa mmekwishafika kwenye ukingoni mwa shimo la jahanamu. Na ikatanabahisha Wakristo na Wayahudi pia ya kwamba nyinyi kwa udanganyifu wenu mmevibadilisha Vitabu vya Mungu. Nanyi mwayatangulia mataifa yote katika kila shari na maovu. Na ikawalaumu pia wayaabuduo masanamu kwamba nyinyi mnaabudu mawe, wanadamu, nyota na vinginevyo na kumsahau Mwumba wa kweli. Nanyi mna kula mali

[15] Aali‘ Imraan, 3:104

ya mayatima, kuua watoto[16] na kuwadhulumu wenzenu, na mmevuka mipaka katika kila jambo.

Vile vile ikasema اِعۡلَمُوۡۤا اَنَّ اللّٰہَ یُحۡیِ الۡاَرۡضَ بَعۡدَ مَوۡتِہَا[17] yaani mtambue jambo hili kuwa ardhi yote ilikuwa imekufa, sasa Mungu Anaihuisha upya. Almuradi, Kurani imeilaumu dunia nzima kwa kosa la ushirikina, ufasiki na ibada ya masanamu ambavyo ni chanzo cha maovu, na ikasema kuwa Wakristo na Wayahudi ni asili ya maovu yote ya dunia, na ikataja kila aina ya maovu yao na kwa kuchora taswira ya matendo ya zama hizo ilionesha kwamba toka iumbwe dunia, hakuna zama zingine zinazofanana na zama hizo pasipo zama za Nuhu[as]. Nasi aya hizi zote tulizoziandika hapa zafanya kazi ya daraja ya kwanza kukamilisha hoja. Hivyo, hatukuziandika aya zote kwa kuhofia kurefusha. Wasomaji wanapaswa kusoma

---

[16] Kama isemavyo ★ یَدُسُّہٗ فِی التُّرَابِ yaani mshirikina humfukia binti yake udongoni. Tena inasema: ☆ وَاِذَا الۡمَوۡءٗدَۃُ سُئِلَتۡ بِاَیِّ ذَنۡۢبٍ قُتِلَتۡ Yaani siku ya Kiyama, mabitni waliozikwa hai wataulizwa, kwamba kwa kosa gani waliuawa? Hapa panaashiria hali ya nchi iliyokwepo kwamba ubaya mwingi wa aina aina unafanyika. Kwenye jambo hili ameashiria mshairi mmoja wa zamani wa Uarabuni aitwaye Ibn Ala'rabi. Amesema:

مَا لَقِیَ الْمَوْءُوْدُ مِنْ ظُلْمِ اُمِّهٖ     كَمَا لَقِيَتْ ذُهْلٌ جَمِيْعًا وَ عَامِرٗ

Yaani, anayezikwa hai hadhulumiwi na mama yake jinsi walivyodhulumiwa Zuhl na Aamir. Mwandishi.

---

[17] Al Hadiid, 57:18 ★ Al Nahl, 16:60 ☆ At-Takwiir, 81:9-10

Kurani Tukufu kwa makini sana, ili wafahamu jinsi Kurani Tukufu kwa nguvu sana na kwa maneno ya kuathiri inavyoeleza kwamba dunia nzima imekwishaharibika, na ardhi yote imekufa na watu wamekwishafika kwenye ukingo wa shimo la jahanamu, na jinsi gani inavyosisitiza mara kwa mara uionye dunia nzima kwamba wamo katika hali ya hatari. Kwa kuisoma Kurani imebainika kwa yakini kuwa dunia imeoza ndani ya ushirikina, uovu, ibada ya masanamu na dhambi za aina aina na imezama katika kisima kirefu cha maovu. Hapana shaka, katika Injili pia mienendo mibaya ya Wayahudi imegusiwa kwa kiasi fulani, lakini Masihi[as] hakuwahi kutaja popote kwamba watu wote waliopo juu ya uso wa ardhi, wanaoweza kutajwa kama walimwengu, wameharibika na kuangamia, na kwamba dunia imejaa maovu na ushirikina, wala hakudai unabii kwa wanadamu wote. Hivyo, ni dhahiri kuwa Wayahudi walikuwa ni taifa dogo lililohubiriwa na Masihi[as] bali hili ndilo liliokuwa mbele ya macho yake na wakazi wa vijiji vichache. Lakini Kurani Tukufu imetaja kufa kwa ardhi nzima na kuelezea hali mbaya ya mataifa yote, na kubainisha kwamba dunia imeangamia kutokana na dhambi ya kila aina.[18] Wayahudi walikuwa kizazi cha manabii na kwa

---

[18] Kama mtu yeyote aseme kwamba zama hizi pia haziko nyuma katika ufisadi, itikadi mbovu na matendo maovu, kwa nini hajaja katika zama hizi Nabii yeyote, basi jawabu lake ni kuwa zama zile

kauli walikuwa wanakiri kuamini Torati, ingawa hawakuweza kuitekeleza, lakini katika zama za Kurani zaidi ya ufasiki na upujufu itikadi pia ziliharibika. Maelfu ya watu walimkana Mungu na maelfu walikuwa wanakataa wahyi na ufunuo, na kila aina ya maovu yalikuwa yameenea ardhini. Na tufani kubwa ya makosa ya kiitikadi na ya kivitendo iliimarika duniani. Isitoshe, Masihi[as] aligusia kidogo baadhi ya maovu ya kaumu yake ndogo ya Wayahudi, jambo lililoleta fikira ya kwamba kaumu mahsusi ya Wayahudi ilihitaji Nabii msuluhishaji. Lakini hoja tunayoieleza kuhusu Mtume[saw] juu ya kuja kwake kutoka kwa Mwenyezi Mungu, yaani ujio wake wakati ufisadi ulipotanda kwa ujumla, na kuitwa kwake baada ya kukamilisha kazi ya usuluhishaji, na Kurani yenyewe kueleza jiha zote hizo mbili na yenyewe kuielekeza dunia kwazo, hili ni jambo lisilokwemo si tu ndani ya Injili bali halimo katika Kitabu kingine chochote cha zamani isipokuwa Kurani Tukufu pekee. Kurani Tukufu yenyewe imeeleza dalili hizi na yenyewe ikaeleza kuwa ukweli wake unathibitika kwa kutazama pande hizi zote mbili. Yaani wa kwanza ni ule tuliokwishagusia kwamba yeye alidhihiri katika zama

---

Tauhidi na unyofu vilitoweka kabisa; lakini katika zama hizi wapo watu milioni 400 wanaosema لَا إِلٰهَ اِلَّا اللّٰهُ (Hakuna apasaye kuabudiwa ila Allah). Hata hivyo Mwenyezi Mungu Hakuzinyima zama hizi kumtuma *Mujadidi*. Mwandishi

ambapo uasi na itikadi mbaya kwa ujumla zilikwishaenea, na dunia ilikuwa imeachilia mbali haki, uhakika wa Tauhidi na utakaso. Na kauli hii ya Kurani Tukufu inathibitika isomwapo historia ya kila taifa ya zama zile, kwa sababu kwa ikirari ya kila taifa hupatikana ushahidi kwa ujumla kwamba nyakati zile kwa hakika zilikuwa za kiza kinene kiasi hiki kwamba kila taifa lilikuwa limeelekea kwenye kuviabudu viumbe. Ndiyo maana Kurani ilipoyalaumu mataifa yote kuwa yamepotea na yametumbukia maovu, hakuna taifa hata moja lililoweza kuthibitisha kujiondolea lawama hizi. Angalieni jinsi Mwenyezi Mungu kwa nguvu Anavyoeleza maovu ya watu wa Kitabu na kufa kwa dunia nzima na kusema:

وَلَا يَكُونُوا كَالَّذِينَ أُوتُوا الْكِتٰبَ مِنْ قَبْلُ فَطَالَ عَلَيْهِمُ الْأَمَدُ فَقَسَتْ قُلُوبُهُمْ ۖ وَكَثِيرٌ مِّنْهُمْ فٰسِقُوْنَ
اِعْلَمُوْٓا اَنَّ اللّٰهَ يُحْيِ الْاَرْضَ بَعْدَ مَوْتِهَا ۚ قَدْ بَيَّنَّا لَكُمُ الْاٰيٰتِ لَعَلَّكُمْ تَعْقِلُوْنَ[19]

(Sura Al-Hadiid, juzu ya 27, fungu la 17). Yaani waaminio wanatakiwa waepukane na mienendo ya watu wa Kitabu, wao walipewa Kitabu hapo kabla. Basi juu yao ulipita muda mrefu, hivyo mioyo yao ikawa migumu na wengi wao ni waovu tu na waasi. Fahamuni jambo hili pia kwamba ardhi ilikwishakufa na sasa Mungu Anaendelea kuihuisha upya. Hizi ni ishara za haja na ukweli wa Kurani zilizoelezwa ili mweze kuzitambua.

[19] Al-Hadiid, 57:17-18

Sasa angalieni kwa kutafakari kwamba hoja hii iliyowekwa mbele yenu hatukuibuni kutoka katika akili yetu, bali Kurani Tukufu yenyewe imeileta. Na baada ya kuzieleza sehemu zote mbili za hoja hii, yenyewe inanena قَدْ بَيَّنَّا لَكُمُ الْاٰيٰتِ لَعَلَّكُمْ تَعْقِلُوْنَ[20] . Yaani, hii vile vile ni ishara tuliyoieleza ya Kitabu hiki na Mtume huyu[saw] kuwa vimetoka kwa Mwenyezi Mungu ili mweze kutafakari, kuelewa na kuufikia uhakika.[21]

[20] Al-Hadiid, 57:18

[21] Maovu yote iliyoyaeleza Kurani Tukufu, ya Wakristo na wengineo waliokuwepo wakati wa kuteremka kwake, waliyakiri hawa wote wenyewe kwa vinywa vyao, bali walikiri mara kwa mara ya kwamba bila shaka wao walikuwa wakiyafanya maovu hayo. Na kwa kuangalia historia ya bara la Arabu, inathibitika ya kuwa mbali na shajara ya nasaba ya Mtume Mtukufu[saw] ambayo Mwenyezi Mungu kwa fadhili na rehema yake mahsusi Aliwahifadhi na ushirikina na mabalaa mengine, watu wengine wote kwa kuona mfano mbovu wa Wakristo na kuathirika na mienendo yao mibaya, walituambukia katika dhambi na maovu ya aina mbalimbali ya kufedhehesha. Maovu na mienendo mibaya iliyowaingilia Waarabu haikuwa matokeo ya tabia zao za asili bali taifa moja chafu na lenye mwenendo mbaya likaja kukaa kati yao ambalo kwa kuitegemea itikadi iliyobuniwa ya kafara, likaiona kila dhambi kuwa ni halali na likaendelea kueneza kwa nguvu zote duniani ibada ya mahuluku, unywaji wa pombe na kila aina ya

Jiha ya pili ya dalili hii ni kwamba Mtume[saw] aliitwa kwenda kwa Mola wake kutoka duniani wakati alipoishakamilisha barabara kazi yake, na jambo hili

---

Mabaki ya Maelezo ya pembeni

maovu na lilikuwa mwongo wa hali ya juu, laghai na lenye khulka mbaya. Kidhahiri ni vigumu kubaini ya kwamba katika zama zile Wayahudi walizidi katika maovu au Wakristo walitangulia. Lakini tukitafakari kidogo, tutagundua kuwa kwa hakika ni Wakristo tu waliokuwa wametangulia katika kila aina ya maovu, mwenendo mbaya na mazoea ya kiushirikina. Sababu yake ni kuwa Wayahudi walikuwa wamedhoofika kutokana na madhila na maudhi ya mara kwa mara. Na zile shari anazoweza kuzifanya mtu duni kwa sababu ya nguvu yake na utajiri wake na kwa kuona upeo wa maendeleo ya taifa lake, au yale maovu yanayotokana na wingi wa mali na fedha, Wayahudi walikuwa wanapata nafasi kidogo ya kuyatenda mambo hayo mabaya. Lakini nyota ya Wakristo ilikuwa inang'aa, na utajiri mpya na utawala mpya ulikuwa unawachochea kwamba yawepo ndani yao mambo yote ambayo daima yanakuwapo kikawaida kwa kuzalika mambo yanayosaidia kutenda maovu. Basi, hii ndiyo sababu ya Wakristo kuzidi katika maovu na maasi katika zama zile. Na jambo hilo ni hakika ijulikanayo kwamba Padre Fandle licha ya chuki yake hakuweza kulificha na akalazimika kukiri maovu ya Wakristo katika kitabu chake Mizanul Haq. Basi wanahistoria wengine Waingereza wameandika kwa mapana na marefu juu ya maovu yao.

linathibitika katika Kurani Tukufu, kama Mwenyezi Mungu Asemavyo: اَلْيَوْمَ اَكْمَلْتُ لَكُمْ دِيْنَكُمْ وَ اَتْمَمْتُ عَلَيْكُمْ نِعْمَتِيْ وَ رَضِيْتُ لَكُمُ الْاِسْلَامَ دِيْنًا★ Yaani leo Nimewakamilishieni dini yenu

---

Mabaki ya Maelezo ya pembeni

Miongoni mwa vitabu hivyo kuna kitabu kimoja cha Bw. Devonport kilichofasiriwa na kuenezwa katika nchi hii. Almuradi huu ni ukweli uliothibitika ya kwamba Wakristo wa zama zile waliwatangulia wote katika maovu kwa sababu ya utajiri wao mpya na utawala wao na itikadi ya kafara yenye madhara. Kila mmoja sawa na tabia yake na mwelekeo wake alikuwa amechagua njia tofauti za kupita kiasi na maasi, na inathibitika kwa kujasiri kwao kwamba wao walikwisha kata tamaa ya ukweli wa dini yao, nao walikuwa hawamwamini Mungu ndani kwa ndani. Na ruhania yao iling'olewa mbali kwa sababu hii hii kwamba milango ya dunia ilifunguliwa kwao. Pombe haikukatazwa katika mafundisho ya Injili, kulikuwa hamna kizuizi chochote kucheza kamari. Basi sumu hizi zote zikijumuika ziliwaangamiza. Masandukuni mlikuwa na mali na mkononi utawala, na pombe wakazivumbua wenyewe,☆ nini tena cha zaidi? Basi wakalazimika kutenda maovu ya kila aina kwa kuchochewa na chimbiko la maovu (pombe). Mambo haya hatukuyasema sisi, bali wanahistoria wakubwa wakubwa Waingereza wametoa ushuhuda wa jambo hili na hata sasa wanaendelea

☆ Kutengeneza pombe kumehesabiwa ni mwujiza wa Yesu, bali kunywa pombe ni nguzo kuu ya dini ya Kikristo, kama ilivyo katika Ekaristi Takatifu (Chakula cha Bwana). Mwandishi

★ Al-Maaida, 5:4

kwa kuiteremsha Kurani Tukufu na kukamilisha nafsi zenu na kuwatimizieni neema Yangu, na kuwapendeleeni Uislamu kuwa dini. Kwa kifupi,

---

Mabaki ya Maelezo ya pembeni

kushuhudia. Padre mkubwa Bosworth na kasisi msomi Bw. Taylor siku hizi wameeleza katika hotuba zao mambo haya kwa uwazi kabisa, na kuthibitisha kwa nguvu sana kuwa maovu ya zamani ya dini ya Kikristo yameiangamiza. Padre Bosworth ambaye ni fahari ya kaumu yake amesema kwa sauti ya juu katika hotuba yake kuwa kaumu ya Kikristo imeambatana na laana tatu zisizotengeka ambazo zinaizuia kupata maendeleo. Hizo ni zipi? Ni uzinzi, unywaji wa pombe na uchezaji wa kamari. Almuradi, ilikuwa ni lazima kwa wakristo kwamba wewe wa kwanza katika nyanja za maovu. Kwani, mtu anaweza kuepukana na dhambi kwa sababu tatu: (1) Awe na hofu ya Mwenyezi Mungu. (2) Wingi wa mali unaosahabisha maovu aepukane na ubaya wake. (3) Aishi maisha ya unyonge na unyenyekevu na asiwe na nguvu ya utawala. Lakini Wakristo walikwisha kuwa huru na vizuizi hivi vyote vitatu na itikadi ya kafara ikawajasirisha kufanya dhambi. Na utajiri na utawala vikawasaidia kufanya dhuluma. Basi kwa kuwa starehe za dunia na neema na utajiri vilikuwa vingi sana kwao na pia walikwishapata utawala wenye nguvu na hapo kabla kwa muda mrefu walikuwa wameishi katika umaskini, njaa na mateso makubwa, kwa hiyo baada ya kupata utajiri na utawala, tufani kubwa ya maovu na maasi ikadhihiri baina

kadri Kurani iliyotakiwa kuteremka imekwisha-teremka na kuleta mabadiliko ya ajabu na ya kushangaza katika nyoyo zilizokuwa macho, na

---

Mabaki ya Maelezo ya pembeni

Na kama vile boma la kuzuia maji linavyobomoka wakati wa mafuriko makubwa na kutokana na kubomoka huku mashamba ya pembezoni mwake na makazi yanapata uharibifu ndivyo ilivyotokea katika nyakati hizo ambapo Wakristo walipata fursa zote na kufanya ufuska na wakawa wa kwanza miongoni mwa wenye nguvu, katika utajiri, nguvu na utawala. Basi kama vile mtu duni aliyechapwa na hali ya njaa na ufukara anavyoonyesha mienendo miovu baada ya kupata utawala na utajiri, ndivyo walivyoonyesha hao. Kwanza wakamwaga damu na kuwaua malaki ya watu bila ya haki wala sababu na wakafanya ukatili unaotetemesha mwili. Nao baada ya kupata usalama na uhuru wakadumu usiku na mchana katika ulevi, uzinzi na kucheza kamari. Na kwa kuwa kwa bahati yao mbaya toka mwanzo itikadi ya kafara iliwajasiri kufanya maovu, na wema wao ulikuwa wa kujisingizia tu na kwa kuwa sasa walitajirika pia, ikawa nini tena! Wakakimbilia kwa kishindo kila uovu jinsi mafuriko yapitavyo kwa nguvu kwa kupata njia wazi, na wakaiathiri vibaya sana mpaka Waarabu wasiozingatia na wasiojua wakasagwa kwa athari yao mbaya. Hao walikuwa hawajui kusoma na kuandika, walipoona tufani ya matendo maovu ya Wakristo pembezoni mwao wakaathirika nayo. Jambo hili limethibitika kwa utafiti wa kina kwamba

kufikisha malezi kileleni, na kuwatimizia neema zake Na hizi ndizo nguzo mbili zinazokuwa shabaha hasa ya kufika kwa Nabii. Sasa angalieni jinsi aya hii

---

Mabaki ya Maelezo ya pembeni

kucheza kamari, ulewi na uzinzi viliingia kati ya Waarabu kutokana na utamaduni wa Wakristo. Akhtal, Mkristo, aliyekuwa mshairi maarufu wa zama zile ambaye diwani yake inaheshimika sana, na siku hizi katika nchi ya Beirut kundi moja la Wakristo limeichapisha kwa shauku kubwa na kuieneza sehemu mbalimbali, na katika nchi hii pia imekwishafika. Katika diwani hii beti kadhaa zimegusia suala hilo, miongoni mwao ubeti mmojawapo ni huu:

بَانَ الشَّبَابُ وَ رُبَّمَا عَلَّلْتُهُ بِالْغَانِيَاتِ وَ بِالشَّرَابِ الْاَصْهَبِ

yaani, ujana umetengana nami, na kwa kuuzuia nilitumia hila kwa kujishughulisha na wanawake warembo na pombe nyekundu. Sasa kutokana na ubeti huu ni wazi ya kwamba mtu huyu juu ya kuwa mzee na kutambulika kuwa mtalamu mkubwa wa Wakristo alizama katika tabia mbaya ya uzinzi. Na jambo la aibu zaidi ni kwamba baada ya kuwa mzee pia hakujizuia na kitendo cha uzinzi, na sio hilo tu bali alikuwa mlevi sana. Watu wanaojua maisha ya Akhtal wanafahamu fika kwamba yeye alikuwa mwenye heshima kubwa katika Wakristo wa zama zile, na katika nyanja za kielimu na kifadhila alikuwa wa pekee. Na kutokana na maandishi yake inadhihirika kwamba sio tu kwamba alikuwa anaeleza mawazo yahusuyo kafara katika ushairi, bali alikuwa na hadhi sawa na ile ya mapadre. Na

inavyoeleza kwa nguvu zote ya kwamba Mtume Muhammad[saw] hakuondoka duniani kabla ya dini ya Uislamu kukamilishwa kwa kuteremshwa

---

Mabaki ya Maelezo ya pembeni

makanisa aliyoyataja katika kitabu chake, inaaminika kwamba yeye alikuwa anaenda huko bila kukosa akiwa kama padre kiongozi, na watu wote walikuwa wanafuata nyayo zake. Je, hoja hii haitoshi ya yeye kuwa wa pekee katika Wakristo wa zama zile kwamba katika mamilioni ya Wakristo na Mapadre ni yeye tu pekee mtu wa zama zile ambaye kumbukumbu yake imepatikana katika miaka elfu ya mia tatu hadi zama hizi. Almuradi, katika Wakristo ni Akhtal peke yake aliyeacha mfano wa mienendo ya Wakristo wa zamani kama kumbukumbu. Sio mfano wake tu mwenyewe, bali yeye ameshuhudia juu ya hali ile ile ya Wakristo wote wa zama zile. Na kwa hakika mwenendo ule ule unaendelea mfululizo mpaka leo hii katika Ulaya. Makao makuu ya dini ya Kikristo yalikuwa nchi ya Kanaani, na kutoka hapo dini hii ikafika Ulaya, na pamoja nayo wakapata zawadi ya maovu yake yote haya. Basi, diwani ya Akhtal inastahiki kuenziwa ambayo imeiondolea pazia mienendo ya Wakristo wa wakati ule. Na historia haiwezi kusema kama Wakristo wanao utungo wowote wa mwingine yeyote kati ya Wakristo wa zama zile. Tutazamapo maisha ya Akhtal twalazimika kuamini kuwa yeye aliifahamu barabara Injili pia, kwa sababu yeye hasa alionesha kati ya Wakristo na mapadre wa wakati ule elimu na uelewa ule ambao hata mmoja

Kurani Tukufu na kukamilishwa kwa nafsi.★ Na hii ndiyo alama mahususi ya kuwa kutoka kwa Mwenyezi Mungu ambayo mwongo hapewi katu.

---

Mabaki ya Maelezo ya pembeni

miongoni mwa Wakristo na mapadre wa wakati huo hakuweza kuuonesha. Kwa vyovyote vile tukalazimika kuamini kuwa yeye alikuwa mfano mteule wa Wakristo wa wakati ule. Lakini sasa hivi mmesikia kuwa yeye mwenyewe akakiri kwa mdomo wake kwamba mimi huondolea majuto ya kuzeeka kwa wanawake warembo na pombe kali. Na hii ilikuwa desturi ya washairi wa wakati ule ya kwamba walikuwa wakielezea ufuska wao kwa maneno haya haya. Na hao walikuwa hawaelezi mawazo ya kubuni ndani ya mashairi kama washairi wasiojua wa siku hizi, bali hao walikuwa wakichora picha halisi ya matukio ya maisha yao. Ndiyo maana machoni mwa watafiti diwani zao hazikupuuziliwa mbali, bali zimepewa daraja barabara ya vitabu vya kihistoria, nazo zinadhihirisha kikamilifu mila, desturi, jazba na fikra za

★ Mwenyezi Mungu Amewaambia masahaba katika Kurani Tukufu kwamba: Mimi Nimekamilisha dini yenu na kuwatimizieni neema Yangu. Na Hakusema hivi ndani ya aya kwamba: Ewe Nabii, Mimi leo nimeikamilisha Kurani. Hekima iliyomo ndani yake ni hii kwamba ili ibainike ya kuwa sio Kurani tu iliyokamilika, bali na wao waliofikishiwa Kurani pia wamekamilika, na shabaha hasa ya utume ikatimia kikamilifu. Mwandishi

Bali kabla ya Mtume[saw], hakuna hata Nabii yeyote mkweli pia aliyeweza kuonesha mfano wa shani ya hali ya juu kama hii kwamba upande mmoja Kitabu

---

Mabaki ya Maelezo ya pembeni

watu wa zamani. Ndiyo sababu wasomi wa Kiislamu hawakuzipoteza kasida na diwani zao ili watu wa kila zama waweze kushuhudia kwa macho yao wenyewe kwamba hali ya Waarabu ilikuwaje kabla ya Uislamu. Halafu baada ya Uislamu kudhihirika, Mungu Mweza Aliwapamba namna gani takwa na utakaso. Kama yakitazamwa mashairi ya Akhtal, Hamasa, Sab‘a Mu‘allaqah na Aghaani aliyoyaandika mwandishi wa Aghaani na yaliyomo katika vitabu vya zamani kama vile Lisanul ‘Arab na Sihaah Jauhari n.k., kisha tukitazama Uislamu kwa kuulinganisha nayo, inaonekana waziwazi ya kwamba katika zama zile za kiza Islam ilidhihirika jinsi jua linavyochomoza mara moja katika kiza kinene. Kwa kuangalia malingalisho haya, onyesho la kudra laonekana wazi, na moyo hupata kupaza sauti kwamba Allahu Akbar, jinsi gani wakati ule kulikuwa na haja ya Kurani Tukufu kushuka. Kwa hakika hoja hii yenye nguvu imewakanyaga chini ya miguu wapinzani wote. Sasa kwa kurejea kwenye mada yetu ya mwanzo twaandika kwamba yumkini mtu asiyejua akauliza swali hili kuhusu Akhtal kwamba kwa nini haijuzu kuwa Akhtal pengine katika uzee wake aliwaoa wanawake wengi warembo; katika hali hii anawezaje kulaumiwa kuzini. Jawabu lake ni kuwa katika ubeti wake, Akhtal hakudhihirisha katu jambo hili kuwa

cha Mungu kikamilike kwa usalama na amani, na upande wa pili nafsi pia zikamilike, na pamoja na hayo kufuru ishindwe kwa kila jiha na Islam ishinde

---

Mabaki ya Maelezo ya pembeni

wale wanawake warembo ni wake zangu. Bali ameeleza katika shairi lake jinsi watu waovu na wazinifu wanavyoeleza siku zote. Ndiyo maana ameunganisha wanawake warembo na unywaji wa pombe nzuri, kwa sababu kunywa pombe ni miongoni mwa mambo ya lazima ya kihuni. Zaidi ya hayo, jambo hili halikufichika kwa yeyote kwamba katika Ukristo kuna ruhusa ya mke mmoja tu. Basi iliwezekanaje watu kumwozeshe mabinti zao vipusa kinyume na dini na desturi yao? Tunakubali kuwa yeye alikuwa bora kielimu na heshima katika kaumu yake yote, na kama vile ilivyo leo heshima ya askofu mkubwa katika kaumu yake, ndivyo alivyokuwa na heshima ya aina hii au zaidi yake, naye alikuwa kiongozi, Imamu na mteule katika watu wote. Sasa iliwezekanaje watu kumwozeshe makusudi mabinti zao visura kinyume na desturi ya zamani. Na ubeti wake huu unatangaza kwa sauti kuu ya kwamba matendo haya maovu yalikuwa yanatendewa naye kiuzinzi tu. Ndiyo maana pamoja nayo uliendelea unywaji wa pombe pia. Je, mtu yeyote anaweza kukubali kwamba kuna mtu mzee, tena yapo mashaka ya ukewenza kwa wenye binti, halafu kuozesha mabinti, mmoja baada ya mwingine kinyume na dini, kinyume na desturi na kinyume na makubaliano ya kijamii, halafu watu waendelee kumwozesha Akhtal

kwa kila jiha. Na sehemu nyingine Alisema: ★ اِذَا جَآءَ نَصْرُ اللّٰهِ وَالْفَتْحُ ۙ وَرَاَيْتَ النَّاسَ يَدْخُلُوْنَ فِيْ دِيْنِ اللّٰهِ اَفْوَاجًا ۙ فَسَبِّحْ بِحَمْدِ رَبِّكَ وَاسْتَغْفِرْهُ ؕ اِنَّهٗ كَانَ تَوَّابًا ☆ Yaani nusra na ushindi uliokuwa umeahidiwa

---

Mabaki ya Maelezo ya pembeni

mabinti zao warembo kwa kufumba macho na wamletee mitungi miwili mitatu ya pombe pia? Pasipo shaka, wazo hili lisilowezekana hakuna anayeweza kulikubali. Uhakika wenyewe ni ule ule tuliokwishauandika ambao mifano yake inapatikana hata leo katika Ulaya, sio mifano mamia wala maelfu bali malaki kwa malaki. Katika matembezi ya nchi za Ulaya uvukapo tu bahari, mandhari hii inaonekana kila mahali. Isitoshe, sio ubeti huu tu wa

---

★ Inadhihirika kutokana na aya hii ya kwamba katika moyo wa Mtume Mtukufu[saw] kulikuwa na jazba kubwa ya kuwa ajionee mwenyewe Islam ikienea katika dunia katika maisha yake mwenyewe, na jambo hili lilikuwa halimpendezi kabisa kwamba aage dunia kabla ya kuistawisha haki duniani. Kwa hiyo katika aya hii Mwenyezi Mungu Anampa Mtume Mtukufu[saw] habari hii njema kwamba: 'Angalia, Mimi nimekidhi utashi wako. Na kila Nabii alikuwa na tamanio hili, kidogo au zaidi, lakini kwa sababu jazba ya daraja hii ilikuwa haipo, kwa hiyo Masihi wala Musa[as] hawakupewa habari hii njema. Bali alipewa yule ambaye kumhusu yeye, Alisemwa katika Kurani Tukufu: لَعَلَّكَ بَاخِعٌ نَّفْسَكَ اَلَّا يَكُوْنُوْا مُؤْمِنِيْنَ ☆☆ Yaani je, utajiangamiza kwa huzuni hii kwamba kwa nini watu hawa hawaamini? Mwandishi.

---

☆ An-Nasr, 110:2-4 ☆☆Ash-Shu'araa, 26:4

umekwishafika, na ukaona watu wanaingia katika dini ya Islam makundi kwa makundi, basi hapo umtukuze Mwenyezi Mungu na kumsifu, yaani sema hivi,

---

Mabaki ya Maelezo ya pembeni

Akhtal, bali kuna ubeti mwingine katika diwani yake unaoushinda ule wa kwanza ambao tunauweka mbele ya wasomaji, nao ni huu:

اِنَّ مَنۡ يَدۡخُلُ الۡكَنِيۡسَةَ يَوۡمًا     يَلۡقَ فِيۡهَا جَآذِرًا وَ ظِبَاءً

Tafsiri ya ubeti huu ni hivi: Kama mtu siku moja akiingia ndani ya kanisa letu, atakuta humo kuna wanapaa na suala, yaani ataburudika kwa kuwaona wasichana wengi warembo, wabichi, wavutiao na wachangamfu. Yaani kana kwamba bwana Akhtal anawahimiza watu lazima waende kanisani ili wapate kuburudika. Sasa kuna mambo mawili yanayoibuka kutokana na ubeti huu. La kwanza ni kwamba Akhtal alikuwa amewajengea watu wake kanisa ambamo yeye alikuwa akienda akiwa padre, na kidhahiri akishika Injili mkononi mwake alikuwa akiwatazama kwa tamaa mabinti na wakwe wa watu huku akiwa ameshajenga nao mahusiano yasiyo halali. Jambo la pili linalodhihirika ni hili kwamba watu walikuwa hawaoni vibabya mahusiano haya yasiyojuzu na wala kumfukuza mwenye kuwatazama wanawake kwa tamaa ya nafsi na wala hawakumwondoa katika cheo chake cha upadre, ilhali wao walikuwa wakitambua kwamba mtu huyu ni mwenye moyo mchafu, na moyoni mwake mna nia ya

kwamba hayo yaliyotokea hayakuwa kwa uwezo wangu bali ni kwa fadhili, ukarimu na msaada wake Yeye, na ufanye Istighfar ya kuagana, sababu Yeye ni

---

Mabaki ya Maelezo ya pembeni

kufanya mabaya. Kwani, beti zake chafu zilizokuwa zinathibitisha tabia yake ya umalaya na uhawara hazikuwa zimefichika kwa watu wake. Basi kutakuwa na dalili gani yenye nguvu zaidi juu ya jambo hili kwamba watu hawa wote walikuwa wametumbukia katika ufasiki na upotevu, na makanisa yao yalikuwa kama madanguro ya makahaba. Na kwa ajili ya wanaume na wanawake wenye mwenendo na tabia chafu hapakuwa na sehemu nzuri zaidi ya kukutana isipokuwa makanisani. Yaani, hao walikuwa wanapata fursa ya kutimiza tamaa zao za nafsi mle kanisani tu. Na Akhtal hakuwa ametumbukia tu katika mtamanio yake mabaya, bali yeye alikuwa hamtambui mwanamke au msichana yeyote wa Kikristo kuwa na utakaso. Hivyo, katika diwani ya Akhtal ambayo pamoja nayo wanazuoni wa Kikristo wamechapisha maisha yake pia ndani yake wameandika katika matukio ya maisha yake kwamba kutokana na swala hili hili la wanawake, safari moja aliwahi kufungwa katika kanisa la Damascus kwa kutuhumiwa kwamba haamini utakaso wa wanawake wa Kikristo. Kisha kutokana na maombi ya Mwislamu mmoja mwema aliyeheshimika, kasisi wa Damascus akamuacha huru. Lakini, Akhtal hakuachana na rai yake hii mpaka kufa kwake. Beti zake zinazohusu wanawake wa Kikristo ni jambo linalovuma hadi sasa. Kwenye

mwelekevu sana kwa rehema. Amri ya kuomba ghofira wanayopewa manabii, kuihusisha na dhambi za watu wa kawaida ni ujinga kabisa. Bali kwa maana

---

ukurasa wa 339 wa kitabu hiki hiki imeandikwa kuhusu maisha ya Akhtal kwamba yeye alikuwa na kawaida ya kuisifu sana pombe katika beti zake na alikuwa anafahamu fika faida za pombe na alikuwa mzoefu sana. Halikadhalika imeandikwa katika kitabu chake cha maisha kwenye ukurasa wa 337 kuwa Akhtal alikuwa Mkristo imara na alikuwa ameshikilia barabara dini yake, alikuwa amekumbuka kikamilifu usia wa kanisa na alikuwa na kawaida ya kuvaa msalaba kifuani kila wakati, ndio maana alikuwa mashuhuri katika watu kwa lakabu ya 'Mwenye Msalaba'. Halafu kwenye ukurasa huu huu imeandikwa kuwa safari moja Sultan Abdul Malik Bin Marwaan ambaye katika baraza lake yeye (Akhtal) alikuwa mfanyakazi, alimshauri kuwa asilimu, akamjibu, "Kama unihalalishie kunywa pombe na kunisamehe kufunga saumu za Ramadhani, mimi niko tayari kuwa Mwislamu". Sasa tazameni, ni punde tu ilisemwa ya kuwa yeye alikuwa Mkristo imara na lakabu yake ni 'Mwenye Msalaba', na mara ikaandikwa kwamba yeye alikuwa tayari kuiacha dini ya Kikristo kwa glasi moja ya pombe. Almuradi katika maisha yake imeandikwa hii hii tu ya kuwa mtu huyu alikuwa mlevi mkubwa na yeye mwenyewe amekiri wazi wazi ya kuwa yeye hawezi kuepukana na mahusiano na wanawake wasiokuwa na mnasaba naye. Na zaidi ya hayo

nyingine, neno hili ni kukiri kwamba hao si chochote na kwamba ni wanyenyekevu na wanyonge, na hii ni njia ya kuomba msaada kwa kujinyenyekeza. Kwa kuwa

---

Mabaki ya Maelezo ya pembeni

amekiri ya kuwa Wakristo wa zama zile, wanaume kwa wanawake, hawakuwa na mwenendo mwema, na ufuska wa siri uliendelea baina yao. Naam, ujasiri wake mkubwa ni huu ya kuwa alithubutu kudhihirisha ufasiki na maovu ya Wakristo na akayaita makanisa yao kuwa sehemu za uzinzi, na pia alikuwa hafichi maovu yake. Imeandikwa katika ukurasa 337 wa kitabu hiki hiki ya kuwa siku moja Abdul Malik alimwuliza, “Unafaidika nini na kunywa pombe?” Mara moja yeye akamsomea beti hizi mbili:

إِذَا مَا نَدِيمِي عَلَّنِي ثُمَّ عَلَّنِي    ثَلَاثَ زُجَاجَاتٍ لَهُنَّ هَدِيرُ

جَعَلْتُ أَجُرُّ الذَّيْلَ مِنِّي كَأَنَّنِي    عَلَيْكَ أَمِيرَ الْمُؤْمِنِيْنَ أَمِيرُ

Yaani, mhudumu wangu wa baa aliponinywesha pombe chupa tatu ambazo wakati wa kuimimina zilitoa sauti ya kupendeza, ndipo katika hali ya kulewa nikaanza kutembea kwa maringo, kana kwamba mimi ndimi Amiri wako, ewe Amirul muminin. Almuradi kwa sababu wakuu wa Kiislamu kwa vyovyote hawakumlazimisha yeyote kusilimu, basi hakuchukuliwa hatua yoyote nyingine zaidi ya kuhubiriwa, naye akaendelea kujizolea zawadi za rupia maelfu katika baraza la wafalme wa ukoo wa Marwaan. Yeye alikuwa amezaliwa katika zama za Mtume wetu Mtukufu[saw] na alipata zama za makhalifa wote wanne (Allah Awaridhie). Aliishi katika nchi ya Siria

imesemwa katika Sura hii ya kwamba kazi aliyoijia Mtume[saw] imekwishakamilika, yaani maelfu kwa maelfu ya watu wameishasilimu, na hii pia inaashiria

---



na akafa akiwa mzee mkongwe. Yeye aliifanya kazi hii nzuri sana ya kuonesha taswira ya mienendo halisi za Wakristo katika beti zake, na kutoa ushahidi ulio wazi kwamba Wakristo wa wakati ule walikuwa wamezama katika mienendo michafu sana nao walikuwa wametawaliwa na unywaji wa pombe na maovu ya aina zote. Na kwa kuwa chimbuko na chanzo cha dini ya Kikristo ni nchi ya Siria ambayo yeye alikuwa mwenyeji wake na ambayo ameonesha picha yake halisi, hii yaonyesha wazi kuwa itikadi ya kafara ni uongo, bure na udanganyifu kiasi gani, ambayo toka mwanzo imethibitika athari yake hii kwamba Wakristo walitumbukia katika kila aina ya ufasiki na uovu. Zama za Akhtal haikuwa mbali sana na zama za Hadhrat Masihi (Yesu). Ilikuwa imepita miaka mia sita tu. Lakini kwa ushahidi wa Akhtal na kukiri kwake mwenyewe inathibitika wazi kwamba Wakristo wa zama zile katika mienendo yao mibaya walikuwa wameporomoka zaidi kuliko walioabudu masanamu. Basi kama itikadi ya kafara ilileta athari hii katika zama za mwanzoni, basi ni wajinga sana wale wanaotarajia mazuri katika karne hii ya kumi na tisa kutokana na itikadi hii hii ya kafara iliyokwishajaribiwa. Kuhusiana na mienendo ya Ukristo wa zama zile kuna ile kasida pia iliyomo katika Sab'ah Mu'alliqah ambayo ni

kwenye kifo cha Mtume[saw], na baada yake Mtume[saw] akafariki ndani ya mwaka mmoja. Basi kutokana na kuteremka kwa aya hii ilikuwa ni lazima kwamba

---

Mabaki ya Maelezo ya pembeni

Muallaqa ya nne, mtunzi wake ni 'Amr Bin Kulthum Taghlibii. Na jambo hili halikufichika kwa mwanahistoria yeyote kuwa Banii Taghlib walikuwa Wakristo nao waliohesabiwa kuwatangulia wote katika ufasiki, uovu, dhulma na ujeuri katika bara lote la Arabu. Basi kasida hii ni ushahidi tosha juu ya mienendo ya Banii Taghlib kwamba namna walivyokuwa mstari wa mbele katika kumwaga damu, kupenda vita, chuki, ufasiki, ulevi na ubadhirifu kwa kutimiza matamanio yao mabaya ya nafsi, na kuona fahari kubwa kwa ufasiki na maovu yao. Hapa kama mfano tunanukuu beti mbili tu za Taghlibii tuliyemtaja, nazo zinapatikana katika kasida ya tano ya ***Sab'ah Mu'allaqah,*** anayependa anaweza kuziangalia humo, nazo ni kama ifuatavyo:

أَلَا هُبِّيْ بِصَحْنِكِ فَاصْبَحِيْنَا    وَ لَا تُبْقِيْ خُمُوْرَ الْأَنْدَرِيْنَا
وَكَأْسٍ قَدْ شَرِبْتُ بِبِعْلَبَكٍّ    وَ أُخْرٰى فِيْ دِمَشْقَ وَ قَاصِرِيْنَا

Yaani ewe mpenzi wangu (mpenzi wake kwa hakika alikuwa mama yake), inuka na bakuli la pombe na ninyweshe pombe zote za kila aina zinazotengenezwa katika mji wa Andariin, na hakikisha kusibaki na pombe yoyote katika stoo zake. Kisha anasema, mimi nimekunywa pombe nyingi katika Ba'labakka, vile vile kiasi hiki hiki nimekunywa katika Demascus na vivyo

Mtume Mtukufu[saw] ahuzunike pia kama alivyofurahia. kwa sababu, bustani lishapandwa, lakini mpango wa kudumu wa umwagiliaji utakuwaje? Hivyo Mwenyezi

---

Mabaki ya Maelezo ya pembeni

hivyo nimekunywa kiasi hiki hiki katika mji wa Qasiriin. Ni ukweli kuwa Wakristo hawakuwa na kazi nyingine zaidi ya kunywa pombe. Hii hii ndiyo nguzo kuu ya dini ya Kikristo ambayo ni sehemu ya Chakula cha Bwana. Lakini jambo la ajabu zaidi kuliko yote ni kwamba Mkristo huyu akawa ashiki wa mama yake. Wasomaji wafahamu ya kuwa Andariin ni mji mmoja katika nchi ya Siria ambamo Wakristo walikuwa wanatengeneza kila aina ya pombe, kisha kuisambaza katika nchi za mbali. Na katika dini yao unywaji wa pombe haukuwa halali tu, bali kama ilivyo katika dhehebu mojawapo la dini ya Kibaniani liitwalo Baam Maargi, unywaji wa pombe ulikuwa sehemu kuu ya dini, ambayo bila ya hiyo mtu hakuweza kuwa Mkristo. Hivyo, toka zamani kumekwapo na uhusiano mkubwa wa Wakristo na pombe, na katika zama hizi pia Wakristo ndio waliobuni pombe za aina aina. Jambo hili limethibitika kuwa Wakristo ndio waliopeleka pombe katika nchi za Kiarabu na kuangamiza. Inaonekana hata wazo la kuabudu masanamu pia limepata nguvu kutokana na fikra ya kumwabudu Kristo. Na kwa kuwaiga Wakristo, watu wa Uarabuni pia wakakomaa katika ibada ya viumbe. Ifahamike kwamba Waarabu wasiostaarabika hawakujua pombe ni balaa gani. Lakini pindi walipofika huko

Mungu kwa ajili ya kuondoa huzuni hii, Akamwamuru kufanya ***Istighfar***. Kwani katika kamusi, maana yake ni kufunika kunakomhifadhi mtu na maafa. Kwa hiyo

---

Mabaki ya Maelezo ya pembeni

Wakristo, waliwapa baadhi ya wafuasi wapya zawadi hii pia, ndipo tabia hii mbaya ikaenea kwa kuigana, na kama vile zilivyo nyakati tano za sala ndivyo zilivyowekwa nyakati tano za kunywa pombe. Yaani ***Jashiriya*** ni pombe inayonywewa asubuhi kabala ya mawio, ***Subuuh*** ni pombe inayonywewa baada ya kuchomoza jua, ***Ghabuuq*** ni pombe inayonywewa wakati wa Adhuhuri na Alasiri. ***Qail*** ni pombe ya saa sita, ***Fahm*** ni pombe ya usiku. Baada ya kuja kwa Islam, ikaleta mabadiliko ya kuwa badala ya nyakati hizi tano za kunywa pombe ikaweka sala tano. Na mahala pa kila uovu ikaweka wema, na badala ya ibada ya mahuluku ikafundisha Jina la Mwenyezi Mungu. Na kuyakana mabadiliko haya matakatifu ni kazi ya mtu duni, si kazi ya mtu mwema. Je, kuna dini yoyote inayoweza kuleta mfano wa mabadaliko mema kama haya? La hasha! Na katika kunukuu beti za kukiri maovu ya Wakristo twaona zatosha kwa sasa. Lakini kama kuna yeyote atakayenung'unika basi mamia kadhaa ya beti za aina hii watapatiwa kama zawadi. Lakini ni imani yangu kuwa hakuna atakayenena lolote sasa. Kwa sababu maelfu ya beti zielezazo ikrari ya maovu zawezaje kufichika?

Sasa mtu amuulize Padre Thakur Das ambaye pasipo haki na kwa chuki pasipostahili, amesema maneno ya

Neno *Mighfar* linalomaanisha helmeti limetokana nalo. Na maana ya kuomba maghufira ni kwamba Mwenyezi Mungu Aizuie kudhihirika ile taabu ama

---

Mabaki ya Maelezo ya pembeni

upuuzi kuhusu kutohitajika kwa Kurani, ya kwamba je hadi sasa bado hajahabarishika kuhusu haja ya ujaji wa Kurani? Au je, sisi hatujathibitisha kuwa Kurani iliteremka wakati ambapo Wakristo wote walikuwa wamekwishaoza kama wale wenye ukoma? Na watu wengine pia wakaangamia kwa kuwapenda. Hii ndiyo haja ya kweli au ile inayoelezwa kuhusu Injili? Yesu amepoteza uahi, na Wakristo wakawa waovu zaidi kuliko hapo kabla. Kama Bw. Thakur Das atapenda, sisi tunaweza kumwambia beti hadi elfu kumi ambamo wapinzani wameyakiri matendo yao maovu. Hata leo pia Wakristo wapo mbele katika baadhi ya maovu. Angalieni tu pombe, "mama wa maovu", kwamba katika mji mmoja tu wa London pekee, maduka ya pombe ni mengi kiasi hiki kwamba ilikadiriwa kuwa kama yatapangwa yote katika mstari mmoja, yatachukua maili 75. Makahaba katika nchi ya Uingereza ni wengi kiasi hiki kwamba katika mji wa London pekee wanaweza wakawa zaidi ya laki moja. Na wamekadiria baadhi ya watu kuwa idadi ya wanaharamu wanaozaliwa mafichoni kwa 'ushujaa' wa wanawake 'watakatifu' inafikia asilimia 75. Mchezo wa kamari ni mwingi mno, Mungu Aepushie mbali! Inaonekana kwamba hofu ya Mungu imetoweka kwenye mioyo ya kaumu hii. Wamemfanya mwanadamu kuwa

dhambi inayohofiwa na Aendelee kuifunikia. Hivyo, kuhusiana na Istighfar hii, ilitolewa ahadi kwamba usihuzunike kuhusu dini hii, Mwenyezi Mungu

---



Mungu, wameyafahamu maovu kuwa mema. Ukweli ni huu ya kwamba fikira ya Masihi kujiua imewaangamiza. Na amri zote za Torati zilizokuwa zinakataza mabaya na zile za kuhimiza mema, zimeondolewa mbali na kafara. Hao wanaichukia Islam kama shetani anavyouchukia ukweli. Hakuna anayefikiria miongoni mwao kwamba Uislamu umeleta jambo gani jipya linalopaswa kupingwa. Nabii Musa[as] aliua maelfu ya watoto, lakini hakuna Mkristo yeyote anayesema kuwa yeye alifanya vibaya. Lakini Seyidi Bwana wetu Mtume[saw] aliinua upanga dhidi ya wale walioinua kwanza panga na akawaua wale waliokwishawawaua kwanza Waislamu wengi, hata hivyo hakuinua upanga mwenyewe isipokuwa wakati makafiri walipowasaka na kuwashambulia. Na hakuwaua watoto wala wazee, bali aliwaadhibu wale tu waliokuwa wahalifu. Wakristo wanaiona vibaya sana adhabu hii. Kila mahali wanaililia hiyo tu. Je haithibitiki kwa hiyo kuwa mioyo yao imekwishakuwa myeusi kwa sababu ya bughudha? Ni jambo la kukera kwamba miili yao haitetemeki kwa kumwita mwanadamu kuwa Mungu, hawaiogopi siku ya kuhojiwa. Kama kwa siku moja Masihi aje baada ya kukufuka, na isemwe, ‘Mwangalieni, huyu ndiye Mungu wenu, shikaneni naye mikono’, hapo watafedheheka sana.

Hataipoteza na daima Ataendelea kuelekea kwake kwa rehema zake na kuzuia mabalaa yanayoweza kuibuka wakati wa udhaifu.

---

Mabaki ya Maelezo ya pembeni

Waabudu viumbe, wenye bahati mbaya, wamewapandisha daraja watu wanyonge baada ya kufa kwao. Hawana haya! Hawamwogopi Mwenyezi Mungu! Wala hawafikirii kwamba Masihi ameonesha nini cha ziada kuliko manabii wengine? Amefanya mambo yepi ya Kiungu? Je, kukesha usiku kucha akilia, halafu dua isikubaliwe, ndio jambo la Kiungu? Akafa akilia Eloi Eloi. Baba hakumhurumia. Matabiri mengi hayakutimia. Miujiza ikatiliwa doa na Ziwa (Galilaya), Mafarisayo wakambana na wakambana sana asiweze kujinasua. Kashindwa kutoa jawabu linalotosheleza katika ufafanuzi wa utabiri kuhusu Eliya. Na hakuweza kumhuisha Eliya kwa ajili ya kutimiza utabiri kwa maneno yake ya dhahiri. Na akaaga dunia akitamka **Lama Sabaktani** kwa majuto makubwa. Mungu wa Mabaniani, Ramchandar, alikuwa afadhali kuliko mungu wa aina hii, aliyeweza kulipiza kiasi katika uahi wake kwa Ravan na hakumwacha mpaka kumwangamiza na kuchoma mji wake. Naam, kafara ulizushwa baadaye, lakini yapasa kuona imeleta faida gani? Wakristo walizidi kuzama katika dhambi. Kuna uovu gani walioepukana nao? Ni uchafu gani ambao hawakushikwa nao? Ni masikitiko kwamba kujiua kumepotea bure. Mwandishi

Wakristo wengi wasioelewa kwa sababu ya kutojua maana halisi ya neno *Maghfira*, wanafikiria kuwa anayeomba maghufira, lazima ni fasiki na mwenye dhambi. Lakini baada ya kutafakari kuhusu neno maghufira, yafamika waziwazi kuwa fasiki na Mwovu ndiye yule asiyeomba maghufira. Kwa sababu, kama kila utakaso wa kweli unapatikana toka Kwake tu naye ndiye Anayemkinga mtu na dhoruba ya tamaa ya nafsi, hivyo muda wote kazi hasa ya waja wa kweli wa Mwenyezi Mungu inatakiwa iwe kumwomba maghufira Yule Aliye Mhifadhi na Mlinzi wa kweli. Tukitafuta mfano wa maghufira katika ulimwengu wa kimwili hatuwezi kupata mfano mzuri mwingine zaidi kuliko boma imara linalojengwa ili kuzuia tufani na mafuriko. Basi kwa kuwa inakubaliwa kuwa uwezo wote na nguvu zote Anazo Mwenyezi Mungu, na mwanadamu kama alivyokuwa mdhaifu kimwili, ni mnyonge kiroho pia, na kwa ajili ya mti wake wa uzima anahitaji umwagiliaji kutoka kwa Yule Aliye wa milele Ambaye bila ya ukarimu wake yeye hawezi kuishi, hivyo *istighfar*, kwa maana yake iliyotajwa, humlazimu hali yake. Na kama vile mti unavyotandaza matawi yake kila upande kana kwamba unanyoosha mikono yake kwenye chemchem iliyo pembezoni mwake na kusema: Ewe chemchem nisaidie, na usinifanye nipungukiwe ustawi wangu na uulinde muda wangu wa kuzaa matunda usipotee, ndivyo ilivyo hali ya watu wanyofu. Kwa ajili ya kuhifadhi ustawi wa kiroho na usalama wake au kwa

lengo la maendeleo yake kuomba maji ya usalama kutoka kwa Chemchem ya uhai wa kweli ni jambo ambalo Kurani Tukufu inaliita ***Istighfar*** kwa maneno mengine. Izingatieni Kurani Tukufu na isomeni kwa makini mkapate uhakika bora wa ***istighfar.*** Na tumekwishaeleza hivi punde kuwa sawa na kamusi, ***Maghfira*** humaanisha kufunika kwa kusudio la kujikinga na afa fulani. Kwa mfano maji ni kitu kimojawapo cha ***maghfira*** kwa ajili ya miti, yaani hufunika aibu zake. Fikirini kuwa kama bustani fulani isipate maji kwa mwaka au miaka miwili sura yake itakuwaje? Je, hii sio kweli kuwa uzuri wake utatoweka moja kwa moja na hatiabaki alama yoyote ya ubichi na uzuri wala haitaleta matunda kwa muda wake, na itaungua ndani kwa ndani, haitakuwa na maua, bali majani yake mabichi na laini yanayopepea yakinyauka yataanguka katika siku chache tu na ukame ukitawala viungo vyake vyote polepole vitaaanza kudondoka kama vya mwenye jedhamu. Kwa nini yataikumba matatizo haya yote? Ni kwa sababu maji yale yaliyokuwa tegemeo la uhai wake, hayakuimwagilia. Mwenyezi Mungu Ameligusia jambo hili pale Aliposema: كَلِمَةً طَيِّبَةً كَشَجَرَةٍ طَيِّبَةٍ[22] . Yaani, neno zuri ni kama mti mzuri. Kama mti mzuri usivyoweza kustawi bila ya maji, ndivyo hivyo maneno mazuri ya mtu mnyofu yanayotoka kinywani mwake yasivyoweza kuonesha uzuri wake kikamilifu wala kustawi mpaka

---

[22] Ibraahiim, 14:25

pale chemchem ile tukufu itakaporutubisha mizizi yao kwa kutiririka katika mfereji wa *Istighfar*. Kwa hiyo, maisha ya kiroho ya binadamu yanaitegemea *Istighfar*, ambayo kwa kupita katika mfereji wake, chemchem ya kweli huifikia mizizi ya ubinadamu na kuiokoa katika kukauka na kuangamia. Dini ambamo haimo falsafa hii, dini hiyo siyo katu kutoka kwa Mwenyezi Mungu. Na mtu yeyote aliyeikengeuka chemchem hii baada ya kuitwa nabii au mtume au mnyofu ama mtakatifu, huyo hakutoka kwa Mwenyezi Mungu. Na mtu kama huyo hatokani na Mwenyezi Mungu katu, bali ametokana na shetani, kwa sababu neno شَيُط (Shait) maana yake ni kufa. Kwa hiyo, yule asiyetaka kuileta chemchem hii kuistawisha bustani yake ya kirho na hakuujaza tele mfereji wa *Istighfar* na chemchem hii, basi huyo ni shetani, yaani ni mtu mwenye kuangamia. Kwa sababu haiwezekani mti wowote uliostawi ubaki hai bila ya maji. Kila mwenye kiburi asiyetaka kuustawisha mti wake wa kiroho na chemchem hii ya uzima, huyo ni shetani na ataangamia kama shetani. Hakuna Nabii mkweli aliyekuja duniani aliyeikengeuka hakika ya *Istighfar* na hakutaka kujistawisha na chemchem hii ya kweli. Naam, Seyidna na Maulana Khatamul Mursaliin, fahari ya watu wa awali na wa baadaye, Muhammad Mteule[saw] akaomba ustawi huu zaidi sana kuliko wote, ndio maana Mwenyezi Mungu Akamstawisha na kumnyunyuzia marashi zaidi kuliko wenzake wote.

Sasa tukirejea kwenye kusudio letu la mwanzo twaandika kwamba kwa hoja hii juu ya Unabi wa Mtume[saw] na ukweli wa Kurani Tukufu kuwa Mtume Mtukufu[saw] alitumwa duniani wakati ambapo hali ya dunia ilikuwa inahitaji msuluhishi mwenye shani kubwa. Naye hakufa wala kuuawa mpaka alipoimarisha ukweli duniani.[23] Alipodhihiri tu akiwa Nabii mara aka-

---

[23] Kidhahiri hapa panazuka pingamizi moja, nalo ni kwamba kama mwenye kuabudu masanamu aseme ingawa tunakubali ya kuwa Mtume Mtukufu[saw] alikomesha ibada ya masanamu, lakini hatukubali kuwa ibada ya masanamu ilikuwa mbaya. Bali tunasema kuwa hii hii ndiyo ilikuwa njia sahihi ambayo Mtume Muhammad[saw] aliizuia. Basi, inaonekana ya kuwa yeye hakuirekebisha dunia bali akaizuia njia sahihi ya usuluhishi. Na vivyo hivyo kama Sabii yeyote aseme kuwa mimi nakubali Mtume[saw] aliondoa ibada ya moto na kufuta ibada ya jua, lakini sitakubali kuwa yeye alifanya kazi nzuri, bali hii hii ilikuwa njia sahihi aliyoifuta. Na kadhalika Mkristo akisema mimi nakubali kwamba Mtume[saw] aliung'oa msingi wa itikadi za Kikristo katika bara la Arabu, lakini siwezi kuhesabu kuwa hii ni namna mojawapo ya usuluhishi na ni kazi njema ya kuzuiwa ibada ya Nabii Isa[as] na mama yake na kuvunjwa misalaba na picha. Bali njia ile ile iliyopingwa ndio iliyokuwa nzuri. Vivyo hivyo kama wacheza kamari, walevi, wazinifu, wauaji wa watoto wa kike, bahili au wabadhirifu, waipendao dhuluma na haina za aina mbalimbali, wezi wadokozi na majambazi, wote walete hoja zao na waseme ingawa sisi tunakubali na kukiri kuwa Islam imezuia

uthibitishia haja yake ulimwengu. Na akalilaumu kila taifa kwa ushirikina, uongo na ya matendo yao maovu, kama Kurani Tukufu ilivyojaa mambo haya. Kwa

---



vizuri njia ya makundi yetu na kufutilia mbali shari zao katika sehemu kubwa ya ardhi kwa kuwaadhibu vikali maelfu ya wezi, lakini kwa ufahamu wetu, watu hao wamefanyiwa dhuluma pasipo haki. Hao walikuwa wanaiba kwa kupata taabu sana na kufanya ujambazi kwa kujitia katika hatari, basi mali yao baada ya bidii kubwa ilikuwa ni halali. Wakasumbuliwa pasipo haki, na desturi ya kale iliyokuwa sehemu ya ibada ikafutwa. Basi majibu kwa makundi haya yote ni kuwa hakuna mtu yeyote miongoni mwa makundi haya atakayejikosoa kwa kinywa chake yeye mwenyewe, lakini baadhi yao ni mashahidi wa wengine. Kwa mfano mtu anayefanya ibada ya Ram Chandar na Krishan Ji na kuwafanya miungu hatajizuia kuwaamini hao kuwa wanadamu tu bali atasisitiza mara kwa mara kwamba ndani mwa watawa hawa wote wawili mlikuwa na mwanga wa Mungu na juu ya kuwa wanadamu walikuwa miungu pia. Na ndani mwao mlikuwa na jiha moja ya umahuluku na jiha nyingine ya Uungu. Na umahuluku wao ulikuwa ni hali mpya iliyoibuka na hivyo sifa zao za kimaumbele kama vile kufa na kusumbuka au kula na kunywa vyote vilikuwa ni hali zilizoibuka tu, lakini Uungu wao ni wa toka azali na sifa za uungu pia ni za tangu azali. Lakini kama waambiwe, kwamba enye Mabwana kama ni hivyo, basi aminini pia uungu wa mwana wa Mariamu, kwani maskini Wakristo wanaolilia jambo hili muda wote basi waburudisheni wao pia, kwa sababu kama mmeamua kufa maji basi kina si kigezo, hapo wanamkadhibisha Hadhrat Masihi kwa kukosa

mfano zingatieni aya hii ambampo Mwenyezi Mungu anasema: ★تَبٰرَكَ الَّذِیۡ نَزَّلَ الۡفُرۡقَانَ عَلٰی عَبۡدِہٖ لِیَکُوۡنَ لِلۡعٰلَمِیۡنَ نَذِیۡرًا Yaani yeye ni mwenye baraka sana aliyeiteremsha Kurani Tukufu juu

---



adabu kiasi kwamba achilia mbali kumwamini kuwa Mungu, wanafika hata kukataa unabii wake pia. Bali wakati mwingine wanafikia kumtukana na kusema kwamba huyu analingana vipi na Shiri Maharaj Barham Muurat Ram Chandar Ji na Krishan Gopal Ruddar; yeye alikuwa ni mtu tu aliyejidai unabii. Hakuna kulinganisha kati ya Shiri Mahraj Krishan Ji na Isa mwana wa Mariamu! Ni la ajabu kwamba kama watawa hawa ma-Avtar wawili wakitajwa mbele ya Wakristo, wao nao pia hawakubali uungu wao, bali wanawasema maneno ya kuwavunjia heshima, ilhali watawa hawa wawili ndio wa kwanza kutambulika kama miungu katika dunia, nao ndio wakuu wa miungu wengine wadogo wadogo, na mwana wa Mariamu na wengine wamejitokeza baadaye na ndio matawi yao. Na Wakristo katika kumfanya Yesu kuwa mungu, wamefuata nyayo za hao waliowafanya watakatifu hawa kuwa miungu, kama vile Kurani Tukufu inavyogusia jambo hili, tazameni aya: وَ قَالَتِ الۡیَہُوۡدُ عُزَیۡرُ ۣابۡنُ اللّٰہِ وَ قَالَتِ النَّصٰرَی الۡمَسِیۡحُ ابۡنُ اللّٰہِ ؕ ذٰلِکَ قَوۡلُہُمۡ بِاَفۡوَاہِہِمۡ ۚ یُضَاہِـُٔوۡنَ قَوۡلَ الَّذِیۡنَ کَفَرُوۡا مِنۡ قَبۡلُ ؕ قٰتَلَہُمُ اللّٰہُ ۚ اَنّٰی یُؤۡفَکُوۡنَ☆ Yaani, Wayahudi wanasema kuwa Uzair ni mwana wa Mungu na Wakristo wanasema kuwa Masihi ni mwana wa Mungu, haya yote ni maneno tu yatokayo midomoni mwao, hawa wanawaiga wale wa kabla yao ambao wakawa makafiri kwa kuwafanya wanadamu kuwa miungu. Walioadhibiwa na Mwenyezi Mungu, wamepindukia wapi? Aya hii inazungumzia wazi wazi kuhusu Wahindi na Wagiriki, na inaeleza

---

★Al-Furqaan, 25:2 ☆At-Tauba, 9:30

ya mtumishi Wake ili awe mwonyaji kwa walimwengu ili awatanabahishe kuhusu njia yao mbaya na itikadi zao mbovu. Basi aya hii ni dalili wazi wazi juu ya jambo hili

---

Mabaki ya Maelezo ya pembeni

kuwa wao ndio wa kwanza waliowafanya watu kuwa miungu, halafu kwa bahati mbaya ya Wakristo mafundiho haya yakawafikia. Hapo wakasema kwa nini tubaki nyuma ya watu hawa, na kwa bahati yao mbaya katika Torati toka mwanzo katika baadhi ya sehemu zake kulikuwa na usemi uliotumika wa kuwaita wanadamu wana wa mungu, bali mabinti wa mungu pia, bali baadhi ya watu wa zamani wakaitwa miungu pia. Na kutokana na dasturi hii hii, katika Injili neno kama hili limetumika kwa ajili ya Masihi pia. Basi neno hili likawa sumu inayoangamiza kwa ajili ya wasiofahamu. Biblia nzima inapaza sauti kwamba neno hili si makhsusi kwa ajili ya mwana wa Mariamu, bali limetumika kwa ajili ya kila nabii na mtu mnyofu, bali nabii Yakubu ameitwa mtoto wa kwanza. Lakini mwanadamu mwenye bahati mbaya anaponasa kwenye utata, hawezi kujinasua. Tena la ajabu zaidi ni kuwa vile vigezo vinavyoelezwa vya Masihi kuwa mungu kwamba yeye ni mungu na binadamu pia, vyote hivi tangu zamani vinapatikana katika vitabu vya Mabaniani kwa ajili ya Krishan na Ram Chandar, na vinafanana na mafundisho haya mapya kiasi hiki kwamba sisi hatuna maoni mengine zaidi ya kusema kwamba haya yote yameigwa kutoka itikadi za Mabaniani. Katika dini ya Mabaniani kulikuwa na itikadi ya utatu (*tare muurti*) uliomaanisha mjumuiko wa Barhama, Bishan na Mahadev. Kwa hiyo Utatu (wa Kikristo) unaonekana umeigwa kutoka katika itikadi kama hii. Lakini jambo la kushangaza ni kwamba kwa ajili ya

kwamba Mtume[saw] alifika katika zama ambapo dunia nzima na mataifa yote yalikuwa yameharibika. Na mataifa pinzani yameshakubali madai haya si tu kwa

---

kumfanya Masihi kuwa mungu na kwa kukwepa vipingamizi vya kimantiki, mbinu wanayofanya Wakristo na kuunga ubinadamu wa Masihi na Uungu, lengo lao ni kukwepa hoja za kimantiki, lakini hata hivyo hawawezi kuzikwepa, na hatimaye hujinasua kwa kusema kuwa hii ni siri ya Mungu. Ndivyo ilivyo taswira ya wale Mabaniani wanaowaita Ram Chandar na Krishan kuwa mungu, yaani wao pia wanatoa maelezo yale yale yanayotolewa na Wakristo. Na wanaposhindwa kwa kila jiha husema hii ni siri ya Mungu ambayo wanaijua wale tu wanaozama katika fikara za Mungu na kujitenga na dunia na kufanya ibada sana.

Lakini watu hawa hawaelwi kwamba siri hii ilifichuka pale tu ambapo miungu hawa wa bandia hawakuonesha mfano wowote wa uungu wao ambao binadamu hakuwahi kuonesha. Hii ni kweli kabisa kwamba katika Ma-Granth visa vya namna hii vimejaa  kwamba Ma-Avtar hao wamefanya kazi kubwa kubwa za nguvu; wakafufua wafu na kubeba milima kichwani. Hata kama tukiviamini visa hivi kuwa kweli, lakini wao wenyewe wanakubali kwamba wako wengine pia walioonesha maajabu kama haya ambao hawakudai kuwa miungu. Kwa mfano, fikirini kidogo na kuangalia kwamba je kazi za Yesu zilikuwa kubwa zaidi kuliko zile alizozifanya Musa? Bali ishara za Yesu zimeharibiwa kabisa na kisa cha bwawa (la Galilaya lililoponyesha wagonjwa). Je ninyi hamjui habari za bwawa hili la miujiza liliokwepo zama zile zile? Na je

kunyamaza bali kwa kukiri kwao. Hivyo imedhihirika waziwazi kuwa Mtume[saw] kwa hakika alifika katika wakati ambapo Nabii mkweli mkamilifu alikuwa

---

katika Waisraeli hawakupita Manabii ambao kwa kuwagusa tu, wafu walifufuka? Basi kuna sababu gani ya majigambo ya uungu wake. Aibu!!!

Ingawa Mabaniani wameandika kazi nyingi kuhusu uwezo wa manabii wao, na wamejaribu bure kuthibitisha uungu wao, lakini visa vyao havina tofauti na vile vya hovyo vya Wakristo. Hata kama idhaniwe kuwa katika hivyo baadhi yao ni vya kweli, hata hivyo binadamu mnyonge aliye na asili ya udhaifu na unyonge hawezi kuwa Mungu. Na ufufuo wa kweli wenyewe ni uzushi na ni kinyume na Vitabu vya Mungu. Naam, ufufuo wa kimuujiza unawezekana ambao hauna maana ya kurudi duniani na kuishi tena duniani lakini si dalili ya Uungu, kwa sababu wanaodai hayo ni wengi. Wamepita wengi waliodai kuwawezesha wengine kuongea na wafu. Lakini jambo hili linaingia katika aina ya "*Kashfe Kubuur*" [hii ni istilahi ya kisufii. Inadaiwa kwamba mtawa akizama kutafakari kuhusu mtu fulani aliyekufa, anaweza kujua habari zake za kaburini) Naam, bila shaka Mabaniani wanayo fadhila moja juu ya Wakristo, nasi pia tunaikubali, nayo ni kwamba wao wametangulia katika kuwafanya watu kuwa mungu, na Wakristo wamefuata walichokibuni Mabaniani. Kwa vyovyote vile hatuwezi kulificha jambo hili kwamba yale yote wayasemayo Wakristo kwa kuzikwepa hoja za kiakili, kwa hakika hawakujifikiria wao wenyewe, bali wameyapora kutoka kwa ma-Shastar na ma-Garanth.

anatakiwa kuja. Na tunapoangalia upande wa pili kwamba Mtukufu Mtume[saw] aliitwa wakati gani, hapo Kurani Tukufu inatuhabarisha wazi wazi kuwa amri ya

---



Mabarhaman walikwishatayarisha tufani hii kubwa kwa ajili ya Karishan na Ram Chandar ambayo imewasaidia Wakristo pia. Basi dhana hii ni batili kabisa kwamba huenda Mabaniani wameyaiba haya kutoka katika vitabu vya Wakristo, kwa sababu maandiko yao haya ni ya zamani ambapo Yesu hakuwepo kabisa juu ya uso wa ardhi. Basi kwa vyovyote tumelazimika kukubali kuwa Wakristo ndio wezi. Hata Bwana Port pia anakubaliana na wazo hili kwamba "Utatu ni matokeo ya fikra potofu kumhusu Plato. Lakini hakika yenyewe ni kwamba Giriki na Bara Hindi zilikuwa katika fikara zao kama vioo vinavyotazamana. Inafikiriwa kwamba malundo ya ushirikina huu wote yalifika Giriki kutoka Bara Hindi kwa njia ya mafundisho ya Veda, na Wakristo majahili wakapora toka humo polepole na kuyatia katika maelezo ya Injli, na (kurekebisha) daftari la matendo yao."

Sasa tunageukia upande wa maana halisi na kuandika kwamba katika dini hizi zote, moja inapoikadhibisha nyingine, basi bila shaka kila moja miongoni mwao kwa maoni yake inaona kuwa urekebishaji wa dunia uko katika kutoweka kwa itikadi ya dini pinzani. Na inaamini kuwa itikadi ya mpinzani wake ni mbaya sana na ni potofu. Sasa kila dini kwa kuiangalia dini pinzani inapokubali uharibifu huu hapo kila dini ikalazimika kukubali kumhusu Mtume[saw] kwamba islahi kwa ujumla ya dunia imefanyika kwa mkono wake yeye, na kwa hakika yeye ndiye aliyekuwa Msuluhishi

kumwita ilitolewa wakati alipokwishatimiza jukumu lake, yaani aliitwa ambapo aya hii ilikwishateremka kuwa ukusanyaji wa mafundisho yote kwa Waislamu ulikwisha-

---



Mkuu. Zaidi ya hayo, watafiti wa kila dini wanakiri kuwa wafuasi wa dini yao wakati huo walikuwa wametumbukia katika maasi na maovu makubwa. Kwa hiyo, Padre Fundal katika "Mizaanul-Haq", mtafiti Port katika kitabu chake na Padre James Cameron Les katika hotuba yake iliyochapishwa Mei 1882, wote wanakiri kuhusu haya maovu. Isitoshe, wanaotambua wema hasa na njia iliyonyooka wanafahamu kwamba dini hizi zote zimetumbukia katika lindi la giza nene,★ na miongoni mwa hawa ambao majahili hao wamewafanya miungu, hakuna hata mmoja aliye Mungu hasa wa kweli. Kwani, alama hasa ya Mungu wa kweli ilikuwa ni hii ya kwamba heshima na utukufu wake vingedhihirika katika matukio ya maisha yake, jinsi mbingu na ardhi zinavyodhihirisha utukufu wa Mungu wa kweli Mwenye nguvu. Lakini alama hii haipo kabisa katika dhati ya miungu hawa maskini na wanyonge. Je akili timamu itakubali ya kwamba yule ambaye atakufa na mwenyewe ni dhaifu ndiye Mungu pia kwa jiha yoyote ile? La hasha! Abadan haiwezekani. Basi Mungu wa kweli ni Yule ambaye sifa zake zisizobadilika zinaendelea kuonekana tangu kale katika kioo cha ulimwengu, na ni Yule asiyekuwa na haja ya kuwa na mwana

---

★ Hii amekiri Pandit Dayanad katika kitabu chae *Satyarath Parkash*, na Bwana Pandit anakubali kwamba India katika zama hizo ilikuwa imekumbwa na ibada ya masanau. Mwandishi.

kamilika, na mahitaji yote ya dini yaliyokuwa yanatakiwa kuteremka yalikwishateremka. Na siyo hii tu, bali pia ilitolewa habari kuwa msaada wa Mwenyezi Mungu nao

---

Mabaki ya Maelezo ya pembeni

ambaye ajiue ili watu wapate wokovu. Bali njia ya kweli ya wokovu toka kale ni moja tu isiyokuwa mpya na ya kubuni, ambayo wenye kuifuata hupata wokovu hasa na matunda yake hapa hapa duniani, na mifano yake ya kweli wanaiona ndani yao. Yaani njia ile hasa ya kweli ni hii ya kwamba kwa kumkubali mwitaji atokaye kwa Mungu wafuate nyayo zake kiasi cha kujifia kwa jiha ya matamanio ya nafsi na kwa njia hii wajitoe fidia yao wao wenyewe. Na hii ndio njia pekee iliyowekwa na Mwenyezi Mungu toka mwanzo katika tabia ya asili ya watafuatao haki. Na toka azali na alipoumbwa mwanadamu na alipojaaliwa utaratibu wa kutoa dhabihu ya kiroho na tabia yake ikawa na utaratibu huu toka mwanzo na kwa ajili ya kukumbusha juu ya utaribu huo zikawekwa pia dhabihu za dhahiri. Huu ndio ukweli ambao Mabaniani na Wakristo wasio na busara na wenye bahati mbaya hawakuuelewa wala hawakuzingatia uhakika wa mambo ya kiroho na wakatumbukia kwenye mawazo mabaya ya kuchukiza na yenye kiza. Mimi sijawahi kushikwa na mshangao sana kwa jambo lolote jinsi ninavyoshangaa juu ya hali ya watu hawa ambao kwa kumwacha Mungu Alie Mkamilifu na Hai na Mzima wa milele na Mhifadhi wa milele wanafuata mawazo potofu na kuona fahari juu yake. Kisha tunarudi kwenye dhamira yetu ya asili na kusema kwamba kama tulivyokwishaeleza hapo mwanzo kuwa usuluhishi wa Seyidna na Maulana na Mtume[saw] ni mkubwa na ni kwa ajili ya wote na unakubaliwa na mataifa yote. Na daraja hii

umefikia ukamilifu wake, na watu wameingia katika Islam makundi kwa makundi. Na aya hizi pia ziliteremka kuwa Mungu Ameimarisha imani na takwa mioyoni mwao na

---



ya usuluhishi hajawahi kuipata Nabii yeyote wa hapo kabla. Na kama mtu afikirie kwa kuweka historia ya bara Arabu mbele yake, yeye atatambua kuwa washirikina, Wayahudi na Wakristo wa zama zile walikuwa wenye chuki kiasi gani na jinsi gani kulikuwa hakuna tegemeo la usuluhishi wao tangu karne kadha. Kisha inueni macho mkaone kuwa mafundisho ya Kurani Tukufu yaliyokuwa dhidi yao namna yalivyoleta athari kubwa na kung'olea mbali itikadi zote mbaya na kila aina ya uovu. Yakaondoa pombe ambayo ni mama wa maovu na yakazuia kucheza kamari, na yakakomesha mauaji ya mabinti na yakarekebisha zile tabia zingine zilizo kinyume na huruma, uadilifu na utakaso wa mwanadamu. Naam, wakosefu wakapata adhabu pia waliyokuwa wanastahiki kuipata kutokana na makosa yao, basi habari ya kazi ya usulihishi si jambo ambalo mtu anaweza kulikataa. Ikumbukwe hapa kuwa baadhi ya mapadre wa zama hizo wafichao ukweli walipoona kwamba usuluhishi sana kwa ujumla umefanywa na mkono wa Mtume[saw] kiasi kwamba hawawezi kuuficha kwa njia yoyote, na kinyume chake usuluhishi uliofanywa na Masihi katika zama zake si kitu chochote, hapo mapadre wakapata wasiwasi kwamba kuwarekebisha waliopotea na kuwafanya waovu kuwa watu wema, jambo lililo alama hasa ya nabii mkweli, jinsi lilivyodhihirika kikamilifu kitimilifu kwa mkonno wa Mtume Mtukufu[saw] , mfano wake hauonekani hata chembe katika usuluhishi wa Masihi, hapo kwa udanganyifu wao wa kidajali

kuwafanya wachukie ufasiki na uovu, nao wakajipatia sifa za khulka tukufu na njema na mabadiliko makubwa yakatokea katka khulka, mwenendo na roho zao. Ndipo

---

Mabaki ya Maelezo ya pembeni

walipojaribu kulificha jua hili ling'aalo, basi wakalazimika kama alivyoandika Padre James Cameron Les katika hotuba yake kwa kuwadangaya watu wajinga kwamba hao watu hapo kabla walikuwa tayari kujirekebisha, na ushirikina na ibada ya masanamu vilikwishakuwa hakiri machoni mwao. 'Lakini kama wenye rai hii ni wakweli katika wazo lao hili, basi hawana budi kuleta ushahidi unaounga mkono wazo lao hili kama vile Kurani Tukufu inavyoleta ushahidi dhidi yao, yaani inasema: اِعْلَمُوْٓا اَنَّ اللّٰهَ يُحْيِ الْاَرْضَ بَعْدَ مَوْتِهَا★ Na kwa kuwaita hawa wote kuwa wafu, kufufuliwa kwao kunanasibisha kwake tu, na sehemu mbalimbali inasema kwamba walikuwa wamenasa katika minyororo ya upotevu na sisi ndio tuliowanasua. Walikuwa vipofu, nasi tukawapa macho ya kuonea; walikuwa kizani nasi tukawajaalia mwanga. Mambo haya siyo yaliyofichika, bali Kurani ikayafikia masikio ya hao wote, nao hawakuyakataa maneno haya, wala hawakudhihirisha kabisa kuwa sisi tulikuwa tayari toka mwanzo, Kurani haikutufanyia hisani yoyote. Basi kama wapinzani wetu wanayo maandiko yoyote yenye pingamizi yanayounga mkono wazo lao yaendeleayo sambamba na Kurani Tukufu kwa karne kumi na tatu, basi wayatoe, waila maneno kama haya ni uzushi wa tabia ya Kikristo na si vinginevyo. Hii ni kauli ya James ambayo imekwishachapishwa katika kitabu "*Madhahibe 'Aalam*", lakini baadhi ya mapadre wa Kikristo wameonesha uhodari zaidi ya huu

★Al-Hadiid, 57:18

baada ya mambo haya yote Sura An-Nasr ikateremka ambayo muradi wake ni kuwa malengo yote ya unabii umekwishatimia na Islam imepata ushindi mioyoni.

---

Mabaki ya Maelezo ya pembeni

wa kuelewa uhakika. Hao wanasema kuwa urekebishaji si jambo lolote, wala hakuna mtu yeyote aliyerekebishwa. Mafundisho ya Torati hayakuwa kwa ajili ya urekebishaji, bali yalikuwa kuashiria kwamba mwanadamu mwenye dhambi hawezi kufauta maamrisho ya Mungu, na mafundisho ya Injili vile vile yalikuwa kwa malengo haya haya, waila kugeuza shavu la pili baada ya kupigwa kofi shavu moja haijawahi kutokea na wala haitatokea, pia wanasema je, Yesu alikuja na mafundisho mapya? Halafu wanajibu wenyewe wakisema kuwa mafundisho ya Injili yalikwepo katika Torati toka mwanzo, na kwa kusanya pamoja sehemu mbalimbali za Biblia hufanyika Injili. Basi kwa nini Yesu alikuja? Kujibu wanasema, 'kwa ajili ya kujiua tu.' Lakini la ajabu ni kwamba Yesu hata kujiua hakupenda na akatamka Eloi Eloi! Lama Sabachthani. Tena hili pia ni la kushangaza kwamba kujiua kwa Zaid kutamsaidia nini Bakri? Kama jamaa wa mtu anaumwa nyumbani kwake, naye kwa sababu ya huzuni yake ajidunge kisu, je, jamaa huyo atapona kwa kitendo chake hiki cha kipuuzi? Au je kama mtoto wa mtu akiugua msokoto wa tumbo, hapo baba yake kwa ghamu hii ajiponde kichwa chake kwa jiwe, je, kwa kitendo hiki cha kijinga, mtoto atapata nafuu?

Na hii pia haieleweki kwamba Zaid atende dhambi na mahala pake Bakri atundikwe msalabani. Mkristo yeyote atuambie kuwa huu ni uadilifu au huruma? Sisi tunakubali kwama kujitoa muhanga au kuwa tayari kutoa uhai kwa ajili ya kheri ya waja wa Mungu, ni

Ndipo Mtume[saw] aliwatangazia wote kwamba Sura hii inaashiria kifo changu. Bali baada yeke Mtume[saw] alifanya hija na kuiita ‘Hajatul Wadaa‘ — Hija ya Kuagana — Na akatoa hotuba ndefu mbele ya kadamnasi akiwa amepanda juu ya ngamia jike, na akasema: ‘Sikilizeni! Enyi waja wa Mungu, mimi nilipata amri hizi kutoka kwa Mola wangu ili nizifikishe hizi zote kwenu, je ninyi mnaweza kushuhudia kuwa mimi nimeshawafikishieni hizo zote? Ndipo watu wote kwa sauti kubwa wakasadikisha kuwa ujumbe wote tumekwishafikishiwa. Hapo Mjumbe[saw] wa Allah akasema akiashiria mbinguni kwa mkono wake mara tatu, ‘Ewe Mungu, Uwe shahidi kwa mambo haya’. Kisha akasema, ‘Mawaidha haya yametolewa kwa sababu huenda mwakani nisiwepo pamoja nanyi’; kisha akasema mara ya pili, hamtanikuta hapa tena. Kisha baada ya kurudi Madina akafariki mwaka wa pili. ★ اَللّٰهُمَّ صَلِّ عَلَيْهِ وَ بَارِكْ وَسَلِّمْ Kwa hakika mambo haya yote yanatokana na Kurani Tukufu, ambayo uthibitisho wake unapatikana kwa mapana na marefu katika historia ya Islam inayokubaliwa.

---

Mabaki ya Maelezo ya pembeni

khulka njema ya hali ya juu kabisa, lakini itakuwa ni ujinga mkubwa kukihesabu kitendo cha upuuzi cha kujiua kuwa khulka ile. Kujiua hivyo ni haramu na ni kitendo cha wajinga na wasio na subira. Naam njia ya kupendeza ya kujibidiisha sana mno inaonekana iking'aa katika maisha ya yule Msuluhishi mkamilifu aitwaye jina Muhammad Mustafa[saw]. Mwandihi

★ Ewe Allah Umsalie na kumbariki na kumpa amani.

Sasa je kuna Mkristo, Myahudi au Baniani yeyote duniani anayeweza kumleta kama mfano msuluhishi wake yeyote wa namna hii ambaye ujio wake utokane na sababu ya mahitaji makubwa ya watu wote na kuondoka kwake kuwe baada ya kutimia malengo yote, na wapinzani waliopelekewa mtume huyo wakiri wenyewe kuwa na hali yao mbaya na matendo maovu. Mimi najua ya kuwa uthibitisho huu mbali na dini ya Kiislamu hakuna kwa dini nyingine. Ni dhahiri kuwa Nabii Musa[as] alikuja kumponda Firauni kichwa na kuwaokoa watu wake, na kuwaongoza kwenye njia iliyonyooka. Alikuwa hahusiki na kuharibika au kutoharibika kwa dunia nzima. Ni kweli yeye aliweza kuwaokoa watu wake na Firauni, lakini hakuweza kuwaokoa katika mkono wa shetani, na wala hakuweza kuwafikisha katika nchi ya ahadi, na wana wa Israeli hawakubahatika kupata utakaso kwa mkono wake; wakaendelea kumwasi mara kwa mara mpaka Nabii Musa[as] akafariki nao wakiwa katika hali ile ile. Na hali ya wanafunzi wa Yesu iko bayana sawa na Injili yenyewe, hakuna haja ya maelezo. Na jambo hili kwamba kwa kiasi gani Wayahudi ambao kwao Yesu alitumwa kuwa nabii waliweza kuongoka katika uhai wake, si jambo lililofichika kwa mtu ye yote. Bali kama unabii wa Yesu upimwe kwa kigezo hiki, basi kwa masikitiko makubwa twalazimika kusema kwamba kwa msingi wa kigezo hiki

unabii wake hauwezi kuthibitika kwa namna yoyote.[24]

Kwa sababu, kwanza, kwa nabii ni lazima aje wakati ambapo kwa dhahiri hali ya kidini ya umati ule anaopelekewa iwe imeharibika kabisa, lakini Yesu hukuweza kuelekeza lawama yoyote kwa Wayahudi inayothibitisha kuwa wao walibadilisha itikadi zao au wamekuwa wezi, wazinifu au wacheza kamari n.k., au wamefuata kitabu kingine baada ya kuachana na Torati, bali yeye mwenyewe alishuhudia kuwa waandishi na Mafarisayo, wamekaa katika kiti cha Musa[as], na Wayahudi wenyewe hawakukiri kuwa waovu na wabaya. Pili, dalili kubwa ya ithibati ya nabii mkweli ni hii kwamba yeye aoneshe mfano mkubwa wa usuluhishi kamili. Hivyo tunapoangalia mfano huu katika maisha ya Yesu ili kuona yeye alileta usuluhisho gani, na ni maelfu mangapi ya watu waliotubu kwa mkono wake lakini sehemu hii pia tunaiktua iko tupu. Naam, wapo wanafunzi kumi na wawili. Lakini tunapoangalia vitendo

---

[24] **Ukumbusho:** Wakristo wanajivunia sana kafara, lakini wale wanaojua historia ya Ukristo wanafahamu fika kwamba kabla ya kujiua kwa Yesu, Wakristo wema waliokuwa wachache sana sawa na Wakristo wenyewe lakini baada ya kujiua kwake boma la kuzuia maovu ya Wakristo likavunjika. Je kizazi hiki cha kafara ambacho leo hii kinapatikana katika Ulaya kinashabihiana kivitendo na wale waliokuwa pamoja na Yesu kabla ya kafara? Mwandishi.

vyao, moyo unatetemeka na tunasikitika sana kwamba hawa watu walikuwa wa namna gani kwamba baada ya kufanya madai makubwa ya ikhlasi waoneshe uchafu kiasi hiki usiokuwa na mfano duniani. Je kwa kuchukua vipande thelathini na kumkabidhi kwa wauaji nabii mkweli na mwongozi mpendwa, huu ndio ulikuwa uhakika wa kuitwa mwanafunzi? Je kulikuwa na ulazima kwamba mkuu wa wanafunzi kama Petro akisimama mbele ya Yesu amlaani, na kwa ajili ya maisha haya mafupi ya siku chache amtusi kiongozi wake mpendwa akiwa mbele yake? Je ilipasa kuwa wakati wa kukamatwa kwa Bwana Yesu wanafunzi wote wamkimbie kwenda zao na wasioneshe subira hata kwa muda kidogo? Je, hizi ndio huwa alama za watu wakweli na waaminifu ambao nabii wao mpendwa anakamatwa ili auawe, walizoonesha wanafunzi wakati huo? Baada ya wao kupita, waabudu mahuluku wakazusha mambo na kuwasifu sana mno, lakini wao jinsi walivyoonesha imani yao katika maisha yao, haya yote yamo katika Injili hadi leo hii. Almuradi ile dalili inayoimarika kwa ajili ya nabii mkweli kutokana na maana ya unabii na utume haikuweza kuimarika kwa ajili ya Yesu. Kama Kurani Tukufu isingetaja unabii wake, basi kulikuwa hakuna njia iliyo wazi kwa ajili yetu ya kumweka katika mnyororo wa manabii wakweli. Yule anayefundisha kwamba mimi ndiye Mungu na Mwana wa Mungu na ambaye sihitaji kuabudu na kutii na ambaye akili yake na busara yake ni kiasi hiki tu kwamba watu watapata

wokovu kwa sababu ya mimi kujiua, je mtu kama huyu anaweza kufikiriwa kuwa mwenye busara na anafuata njia iliyonyooka? Lakini twamshukuru Mwenyezi Mungu kwamba mafundisho ya Kurani Tukufu yametueleza bayana kuwa haya yote ni masingizio ya uongo kwa mwana wa Mariamu. Katika Injili hamna ishara yoyote ya Utatu. Ule msemo wa kwaida wa "mwana wa Mungu", uliotumika toka zamani katika Vitabu vya kale kwa ajili ya watu maelfu toka zama za Adamu mpaka mwisho, msomo uo huo wa kwaida umetumika katika Injili kwa ajili ya Yesu. Kisha wakapiga chuku hadi Yesu akawa mungu kwa msingi wa msemo huu huu, ilhali Yesu hakuwahi kudai Uungu wala kutamani kujiua wakati wowote, kama Mwenyezi Mungu alivyokwishasema kuwa kama angefanya hivyo jina lake lingeondolewa kutoka katika daftari la wakweli. Pia ni vigumu kukubali kuwa msingi wa uongo huu wa aibu umezushwa na upotevu wa fikara za waanfunzi. Ingawaje hata kama ni sawa yaliyoandikwa katika Injili kuwahusu hao kwamba hao walikuwa na akili hafifu na wepesi wa kukosea, lakini hata hivyo hatuwezi kukubali kwamba wao baada ya kukaa na nabii walikuwa wanaeneza mawazo ya kipuuzi kama haya. Lakini kwa kuyaangalia kwa makini maelezo ya Injili inaomkana ukweli huu kuwa ujanja huu wote ni wa Paulo ambaye ameutekeleza kwa hila kubwa kama wafanyavyo wanasiasa wajanja.

Almuradi, yule mwana wa Mariamu ambaye Kurani Tukufu imetupasha habari zake, aliwajibika kushikamana na mwongozo ule ule wa zamani ambao toka mwanzo uliwekwa kwa ajili ya Nabii Adamu. Hivyo, ushahidi wa Kurani Tukufu juu ya unabii wake unatosha sana hata kama sawa na Injili kuwe na shaka na wasiwasi kiasi gani juu ya unabii wake.

وَالسَّلَامُ عَلٰى مَنِ اتَّبَعَ الْهُدٰى[25]

Mwandishi
Mnyenyekevu
Ghulam Ahmad.

---

[25] Amani iwe juu ya yule afuataye mwongozo.